# Nipashe

Jumatano Mei 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580956

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS
CHEZA JACKPOT
TZS 222,883,040
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Majaliwa** amsimamisha kazi Mkurugenzi wa Halmashauri Jiji la Arusha

UKURASA 7



MBAPPE ATOA SABABU KUTAKA KUTUA LIVER

UKURASA 21

# Rais Liberia afichua siri Samia kung'ara

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza katika mdahalo pamoja na baadhi ya viongozi wakuu wa nchi nyingine kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa 57 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), jijini Accra nchini Ghana jana, kujadili fursa mbalimbali pamoja na changamoto zinazolikabili Bara la Afrika. Kushoto ni Rais wa Ghana, Nana Akufo-Addo na Makamu wa Rais wa Ivory Coast, Tiémoko Meyliet Koné. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**DIWANI ALIYETOWEKA MIEZI MITATU APATIKANA**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limefanikiwa kumpata Diwani wa Kawe, Mutta...

## Adaiwa kumchinja mke, mtoto miaka minne akishuhudia

UKURASA 3



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Juma Kipanga (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Idara ya Ubunifu wa Benki ya NMB, Proches Kachenje (katikati), alipotembelea banda la NMB, baada ya kuzindua Wiki ya Ubunifu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja wa benki hiyo, tawi la Chuo Kikuu, Kingsley Chilambo. Benki ya NMB ndio mdhamini wa maonyesho hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mgawo mabilioni ujenzi wa barabara hadharani

UKURASA 2

MICHEZO **MABEKI YANGA WAWEKWA KITIMOTO** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Daniel Chongolo (kushoto), akizungumza na Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa nchini, Sisty Nyahoza (kulia) na baadhi ya wajumbe wa kikosi kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa Tanzania, alipofika katika ofisi ndogo za Bunge jijini Dar es Salaam jana kuwasilisha mapendekezo ya chama hicho juu ya muundo wa siasa za vyama vingi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Liberia afichua siri Samia kung'ara

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan yuko jijini Accra, Ghana kutunukiwa tuzo maalum, Rais mstaafu wa Liberia, Ellen Johnson Sirleaf, amesema mafanikio ya kiongozi huyo wa Tanzania ni zao la nguvu ya mabega ya viongozi wanawake wanapokuwa madarakani.

Rais mstaafu Sirleaf ametaja yanayomgusa yanajumuisha Rais Samia kuwa kati ya wachache waliohutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN), pia miongoni mwa viongozi wanawake waliopatikana kidemokrasia.

Amemsifu Rais Samia aliyeko jijini huko kwa ziara ya kikazi ya siku tatu itakayoendana na kutunukiwa tuzo ya Babacar Ndiaye, kwamba ameuonyesha ufanisi huo kwa vitendo.

Sirleaf aliyeiongoza Liberia kwa miaka 12 kati ya 2006 na 2018, jana alimrejea Rais Samia kuwa katika orodha ya watu 100 wenye ushawishi duniani kwa mwaka huu kwa mujibu wa jarida la TIME la Marekani.

"Mnamo Septemba 2021, miezi michache baada ya urais, Samia alitoa hotuba ya kihistoria kama kiongozi wa tano wa Kiafrika aliyewahi kuhutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

"Alisimama mahali niliposimama miaka 15 iliyopita kama Rais wa kwanza mwanamke aliyechaguliwa kidemokrasia barani Afrika. Kama Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya nchi yangu, mzigo wa matarajio ya kuleta usawa wa kijinsia ni mzito zaidi kwenye mabega yangu," alisema.

Baadhi ya watu maarufu waliotajwa kwenye jarida hilo ni pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Apple, Tim Cook, Mwimbaji, mtunzi na mwigizaji wa Marekani, Mary J. Blige, mcheza sinema wa Canada, Simu Liu, mcheza mpira maarufu wa kikapu Marekani, Candace Parker na mwanasiasa na mwigizaji wa Ukraine, Volodymyr Zelensky.

Sirleaf ambaye pia amewahi kuwa mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Samia kumekuwa na mabadiliko makubwa Tanzania baada ya kufunguliwa mlango wa mazungumzo kati ya wapinzani wa kisiasa. Alisema hatua zimechukuliwa ili kujenga upya imani katika mfumo wa kidemokrasia, juhudi zimefanywa kuongeza uhuru wa vyombo vya habari, na wanawake na wasichana wana mfano mpya wa kuigwa.

Sirleaf alisema Rais Samia alipozungumza maneno yenye nguvu kwenye Baraza Kuu la UN, hakuweza kujizuia kufikiria jinsi mabega ya viongozi wanawake yalivyo na nguvu na ni kiasi gani wanaweza kuleta mabadiliko.

Akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika uliofanyika jana Accra, Ghana, Rais wa nchi hiyo, Nana Addo Dankwa Akufo-Addo, pamoja na mambo mengine, alisema wakati umefika kwa nchi za Afrika kupigana vita vya kiuchumi kwa maslahi ya bara hilo.

"Rasilimali zetu zimenufaisha wakopeshaji wa kigeni kwa muda mrefu sana huku tukigharamika vibaya kwenye soko la mitaji la kimataifa, wakati rasilimali zetu zilikuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi ya mataifa ya magharibi," alisema.

Aliongeza kuwa ni wakati nchi za Afrika kuondoa vikwazo vya kimuundo vinavyozuia maendeleo ya bara hilo pamoja na kushughulikia ukwepaji wa kodi na shughuli haramu zinazofanywa na mashirika ya kimataifa ambayo yanazuia maendeleo ya bara hilo.

"Afrika lazima itumie uwezo wake wa uzalishaji kwa pamoja na kujenga uwezo kwa benki za maendeleo za bara ili kutambua Afrika tunayoitaka na zaidi," alisema.

Akizungumzia athari za mabadiliko ya tabianchi, Rais huyo alisema benki zinatakiwa kuiwezesha Afrika katika safari ya kutafuta nishati safi katika njia ambayo haiathiri uoto wake wa asili.

"Kwa mantiki hiyo, ndiyo maana ninasema mkutano huu utumike vizuri, mwisho wa mkutano Afrika inatarajia mfumo wa kupatanisha watu na hali ya hewa kwa amani, hatuwezi kuwaangusha watu na sayari, ni lazima vyote vishinde na ili hili lifanyike, lazima Afrika ishinde," alisema.

**KAULI YA SAMIA**

Akizungumza katika mkutano huo, Rais Samia alisema shida anazozipitia katika uongozi wake, ni sehemu ya yaliyomjengea imani kwa Watanzania kwamba anaweza kuongoza nchi hiyo kama ilivyo kwa Rais mwanamume.

"Changamoto ya kwanza ilikuwa ni imani, kuwafanya Watanzania waniamini kuwa ninaweza kuongoza nchi kama vile wanaume, kwa hiyo ilibidi niwathibitishie kuwa ninaweza.

"Wanawake hawawezi kushindwa, na ninafikiri ndani ya mwaka mmoja nilionyesha nguvu ya mwanamke," alisema Rais Samia huku akishangiliwa na waliohudhuria mkutano huo.

Alikitaja kikwazo kingine kwake ni kuongoza nchi kipindi ambacho dunia imekumbwa na janga la maambukizi ya UVIKO-19 lililosababisha uchumi kuyumba, uchumi wa Tanzania ukishuka kutoka asilimia 6.8 mpaka nne.

# Mgawo fedha za ujenzi barabara utakavyokuwa

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 61.585 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mikoa zenye urefu wa kilometa 734.59 na madaraja katika mwaka ujao wa fedha.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alibainisha hayo bungeni jijini hapo juzi alipowasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ukarabati wa jumla ya Km 672.77 kwa kiwango cha changarawe, kujenga Km 61.82 kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja/makalavati 31.

Kwa mujibu wa waziri huyo, barabara zinazotarajiwa kufikiwa na mpango huo ni Mwanza/ Shinyanga Border–Mwanza (Km 102), Sh. milioni 385 zikitengwa kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanyia ukarabati na kuondoa msongamano barabara za Dar es Salaam (km 138.5), wakitenga Sh. bilioni 5.105 kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi wa barabara.

Aliwataja makandarasi watakaolipwa kuwa ni wa baraza za Mbezi-Malambamawili-Kinyerezi-Banana (Km 14), Mbezi Mwisho–Goba (Km 7), Tangi Bovu-Goba (Km 9), Kimara Baruti–Msewe–Changanyikeni (Km 2.6), Banana-Kitunda-Kivule-Msongola (Km 14.7).

Pia sehemu ya Kitunda-Kivule (Km 3.2), Ardhi-Makongo-Goba; sehemu ya Goba-Makongo (Km 4), Tegeta Kibaoni-Wazo Hill-Goba-Mbezi/Morogoro, sehemu ya Madale-Goba (Km 5); Tegeta Kibaoni-Wazo Hill-Goba-Mbezi/ Morogoro Road (Mbezi Mwisho) na sehemu ya Wazo Hill-Madale (Km 6).

Waziri huyo alisema wataendelea na ujenzi wa barabara ya Ardhi-Makongo-Goba; sehemu ya Ardhi-Makongo (Km 5) na kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba-Kisopwa-Kwembe-Makondeko (Km 14.66); sehemu ya Mloganzila-Mloganzila Citizen (Km 4.0).

Vilevile, Kongowe–Mjimwema-Kivukoni Ferry Road (Km 25.1), Mji Mwema-Kimbiji-Pembamnazi (Km 27) na Goba-Matosa-Temboni (Km 6) pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (Km 9.1).

Prof. Mbarawa alisema barabara ya Nyamuswa-Bunda-Kisorya (Km 107.4) imetengewa Sh. bilioni 2.01 kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi na mhandisi mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Kisorya-Bulamba (Km 51) na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyamuswa-Bunda-Bulamba (Km 56.4).

Kwa mujibu wa waziri huyo, barabara ya Kolandoto-Lalago-Ng'oboko-Mwanhuzi (Km 122) imetengewa Sh. bilioni mbili (fedha za ndani) kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Prof. Mbarawa alisema barabara ya Ndundu-Somanga (Km 60) imetengewa Sh. bilioni 2.1 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya mkandarasi na kuanza maandalizi ya ukarabati wa barabara za Kongowe-Malendego (Km 160.65) na Nangurukuru-Mbwemkuru (Km 95).

"Barabara ya Kasulu-Manyovu (Km 68) imetengwa Sh. milioni 600 - fedha za ndani na Sh. bilioni 11.4 - fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wake na barabara za kuingia mjini Kasulu (Km 68).

Sh. bilioni 4.9 - fedha za ndani na Sh. bilioni 31.9 - fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje katika Jiji la Dodoma sehemu ya Nala-Veyula-Mtumba-Ihumwa Dry Port (Km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port-Matumbulu-Nala (Km 60).

"Fidia kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mzunguko wa ndani Dodoma (Dodoma Inner Ring Road) kwa sehemu ya Bahi R/About-Image R/About-Ntyuka R/About-Makulu R/About (Km 6.3).

"Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya mzunguko wa kati katika Jiji la Dodoma inayoanzia Nanenane-Miyuji-Mnadani Sekondari-Mkonze-Ntyuka-Nanenane (Km 47.2) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kikombo Jct-Chololo-Mapinduzi (JWTZ HQ) (Km 18)," alibainisha.

Alisema barabara ya Kidatu-Ifakara-Lupilo-Malinyi-Londo-Lumecha/Songea (Km 499) imetengewa Sh. bilioni 4.6 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu-Ifakara (Km 66.9) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara-Lupilo-Malinyi-Londo-Lumecha (Km 396) na Chalinze-Magindu-Lukenge-Seregete B-Kabwe Jct-Mkulazi (Km 77.5).

"Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Mpanda-Mishamo-Uvinza; sehemu ya Vikonge-Uvinza (Km 159), Kibaoni-Sitalike (Km 71) na Kagwira-Ikola-Karema Port (Km 112). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kizi-Lyambalyamfipa-Sitalike (Km 86.31) na Lyazumbi-Kabwe (Km 65)," alisema.

Prof. Mbarawa alitaja barabara nyingine ni ya Nyanguge-Musoma/ Usagara-Kisesa Bypass (Km 214.25), ikitengewa Sh. milioni 530 kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya makandarasi wa barabara za Simiyu/Mara Border-Musoma (Km 85.5) na Usagara-Kisesa (Mwanza Bypass Km 17.35).

"Barabara ya Mwigumbi-Maswa-Bariadi-Lamadi (Km 121) zimetengewa Sh. bilioni 1.22 kwa ajili ya kulipa madai ya makandarasi na wahandisi washauri wa barabara za Mwigumbi-Maswa (Km 50.3) na Maswa-Bariadi (Km 49.7)," alisema.

*SOMA HOTUBA UK. 11-16

## HABARI KITAIFA

# Adaiwa kumchinja mkewe, mtoto miaka 4 akishuhudia

**Na Anjela Mhando,** SIHA

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linamshikilia mkazi wa Kijiji cha Ndinyika, Kata ya Karansi wilayani Siha, Stephano Sikawa (33), kwa tuhuma ya kumchinja hadi kumuua mkewe, Sioni Daudi (26), mbele ya mwanawe mwenye umri wa miaka minne.

Inadaiwa kuwa mtuhumiwa wa mauaji hayo ametekeleza unyama huo kwa kumkata sehemu zake za siri na kuchukua kiungo hicho, akakata viganja vya mkono wa kulia, vidole viwili na kumtoboa macho mwenzi wake huyo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi Simon Maigwa, Sioni aliuawa na mumewe juzi akiwa nyumbani kwake kijijini huko.

"Ni kweli nimepokea taarifa kuhusu mauaji hayo ya kikatili. Mume wa marehemu imebidi tumkamate kwa sababu anahusishwa na mauaji hayo. Kuna rekodi ya maneno yake aliyokuwa akiyasema huko nyuma kwamba atamfanya kitu kibaya.

"Alikuwa ni mtu na mpenzi wake na ni watu ambao walikuwa na wivu wa mapenzi. Sasa hivi Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa pamoja na Polisi Dawati la Jinsia la Wilaya na OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya) wako wanafuatilia sakata hilo," alisema.

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Ndinyika, Joseph Laizer, alikiri mauaji kutokea usiku wa kuamkia juzi.

"Sisi wananchi tumefahamu kuhusu mauaji hayo majira ya saa 1:08 juzi usiku baada ya mtoto wa marehemu aitwaye... (anataja jina la mtoto mwenye umri wa miaka minne), kushuhudia mauaji na kutoka ndani.

"Alituambia mama yake yuko... (alitamka neno lililomaanisha hakuwa na nguo) na amelala mlangoni. Hayo maneno alimwambia babu yake mdogo ambaye ni jirani kuwa mama yake amelala chini, akimwamsha haongei," alisema.

Tukio hilo ni mwendelezo wa matukio mengi ya mauaji ya kikatili yanayoripotiwa nchini, mwanzoni mwa mwaka huu kukishuhudiwa matukio mengi ya aina hiyo.

Viongozi wa dini na wadau wa haki za binadamu, wakiwamo wabunge na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) wameshapaza sauti dhidi ya matukio hayo, wakitaka hatua zichukuliwe serikalini na jamii kwa ujumla kudhibiti hali hiyo.

# TRA yatoa siku saba kampuni kulipa mil. 308.5/-

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kodi ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar imetoa siku saba kwa Kampuni ya Turkys Mifuko inayomilikiwa na mfanyabiashara Toufky Salum Turky, kulipa kodi ya Sh. milioni 308.5 baada ya msamaha wa kodi wa gari ya kifahari aina ya Benzi kukataliwa na Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Naibu Kamishna wa Mamlaka hiyo, Juma Hassan Juma, alisema wamelazimika kuchukua hatua hiyo baada ya Waziri wa Fedha kueleza maombi ya msamaha wa kodi yaliombwa kinyume na sheria kabla ya gari kutolewa kwa bodi ya dhamana ya Bima.

Juma alisema tayari kampuni hiyo imeandikiwa barua kuhakikisha wanafika TRA kukamilisha malipo na iwapo watashindwa kujitokeza baada ya muda waliopangiwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Kama watashindwa kulipa muda wa siku saba kumalizika TRA tutachukua hatua za kisheria kwa kutumia dhamana ya Bodi ya bima ambayo waliweka kabla ya gari kuruhusiwa kutoka kupitia Bandari ya Malindi Zanzibar," alisema Naibu Kamishna Juma.

Alisema maombi ya msamaha wa kodi hiyo yametupwa kwa mara ya pili baada ya awali wahusika kukata rufani Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), wakipinga uamuzi wa aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Jamali Kassim Ali, kabla ya kutupwa tena na Waziri wa Fedha.

"Kwa mujibu wa barua ya ZIPA ya kuwatetea wapewe msamaha wa kodi walisema kama wawekezaji wanastahili kupewa msamaha wa kutolipa kodi na waziri," alisema Naibu Kamishna huyo.

Hata hivyo, alisema mamlaka za kusimamia sheria zinapotoa uamuzi zinapaswa kutekeleza kwa mujibu wa sheria na sio utashi wa mtu binafsi ili kuepusha uvunjifu wa sheria.

Alisema TRA itahakikisha fedha hizo zinalipwa na wahusika ili kulinda mapato ya serikali kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za kusimamia sheria Zanzibar.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja Uhusiano na huduma kwa walipa Kodi Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Makame Mohamed Khamis, alisema baada ya uamuzi wa waziri, wahusika wanatakiwa sasa kukamilisha taratibu za kulipia kodi kabla ya gari hilo kupewa kadi ya umiliki.

Hata hivyo, alisema gari imepewa usajili wa namba Z-1 baada ya kulipa gharama ya Sh. milioni 15, lakini hairuhusiwi kutembea barabarani kwa sababu ni kinyume na sheria.

## TAARIFA KWA UMMA

NSSF — Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

### PUNGUZO LA TOZO (GHARAMA) ZA KUVUKA DARAJA LA NYERERE (KIGAMBONI)

**Dar es Salaam, 22 Mei 2022**

Kufuatia agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, alilolitoa tarehe 6 Desemba 2021 kuhusu kufanya mapitio ya tozo za Daraja la Nyerere, Mfuko unapenda kuwatangazia wananchi wote kwamba, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa mujibu wa Kifungu cha 61 (1) na (2) cha Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007, ameridhia viwango vipya vya tozo katika Daraja la Nyerere.

Viwango vilivyoainishwa katika Jedwali hapa chini vimeridhiwa kuanza kutumika kuanzia tarehe 20 Mei 2022:

| Na. | Aina ya chombo cha usafiri | Tozo za zamani kwa safari 'trip' moja (TZS) | Tozo mpya kwa safari 'trip' moja (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Watembea kwa Miguu | Bure | Bure |
| 2 | Baiskeli | Bure | Bure |
| 3 | Bodaboda | 600.00 | 300.00 |
| 4 | Bajaji | 1,500.00 | 500.00 |
| 5 | Magari Madogo aina ya Saloon, Station Wagon na Pick up | 1,500.00 - 2000.00 | 1,500.00 |
| 6 | Mabasi ya Daladala yanayobeba abiria wasiozidi 15 | 3,000.00 | 1,500.00 |
| 7 | Mabasi ya Daladala yanayobeba abiria kati ya 15-41 | 5,000.00 | 3,000.00 |
| 8 | Mabasi Makubwa yanayobeba abiria zaidi 41 | 7,000.00 | 4,000.00 |
| 9 | Magari ya Mizigo/Malori kulingana na aina na uzito wa gari | 7,000.00-75,000.00 | Inabaki kama ilivyo sasa |

Aidha, Waziri ameridhia viwango vipya vya tozo kwa watumiaji watakaopenda **kulipa kwa siku, wiki au kwa mwezi** kwa vyombo vya moto vya aina zote (magari ya mizigo/malori kulingana na uzito wa gari, magari madogo aina zote, bodaboda na mabasi ya Daladala ya aina zote) vinavyotumia Daraja la Nyerere kama vinavyoonekana katika Jedwali hapa chini. **Tarehe rasmi ya kuanza kutumika kwa viwango hivi itatangazwa kabla ya mwisho wa Mwezi Juni 2022.**

| Na. | Aina ya chombo cha usafiri | Tozo kwa siku (TZS.) | Tozo kwa Wiki (TZS.) | Tozo kwa Mwezi (TZS.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Watembea kwa Miguu | Bure | Bure | Bure |
| 2 | Baiskeli | Bure | Bure | Bure |
| 3 | Bodaboda | 500.00 | 2,000.00 | 5,000.00 |
| 4 | Bajaji | 3,000.00 | 10,000.00 | 20,000.00 |
| 5 | Magari Madogo aina ya Saloon, Station Wagon na Pick up | 2,500.00 | 12,000.00 | 35,000.00 |
| 6 | Mabasi ya Daladala yanayobeba abiria wasiozidi 15 | 10,000.00 | 30,000.00 | 80,000.00 |
| 7 | Mabasi ya Daladala yanayobeba abiria kati ya 15-41 | 20,000.00 | 80,000.00 | 200,000.00 |
| 8 | Mabasi Makubwa yanayobeba abiria zaidi 41 | 20,000.00 | 110,000.00 | 320,000.00 |
| 9 | Magari ya Mizigo/Malori kulingana na aina na uzito wa gari. | Punguzo la Asilimia 10 | Punguzo la Asilimia 20 | Punguzo la Asilimia 20 |

Imetolewa na:

Lulu Mengele
**Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma (NSSF)**

Tanzania SENSA 2022 Jiandae Kuhesabiwa

@NssfTanzania | +255 756 140 140

# Watatu walivyopoteza maisha ajalini Kahama

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WATU watatu wamefariki dunia na 26 kujeruhiwa katika ajali ya basi la kampuni ya Ruksa lenye namba za usajili T 625 ARJ linayofanya safari zake kati ya Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama kwenda Kaliua mkoani Tabora.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya Kahama, Dk. George Masasi, alikiri kupokea maiti tatu na majeruhi 26.

Dk. Masasi alisema alipokea majeruhi 26 na maiti tatu huku watu wawili ambao walijeruhiwa hali zao zikiwa mbaya.

Kutokana na majeruhi hao kuwa na hali mbaya alilazimika kuwapa rufani ya kwenda Hospitali ya Kanda ya Ziwa ya Bugando, mkoani Mwanza.

Alisema watu wanane kati ya majeruhi hao walitibiwa na kuruhusiwa kuondoka na 18 waliendelea kulazwa na kupatiwa matibabu.

"Waliopatiwa rufaa kwenda Bugando mmoja aliumia maeneo ya kichwani na mwingine kuvunjika mkono wa kushoto," alisema Dk. Masasi.

Mmoja wa majeruhi hao aliyeumia mkoni na kifua, Regina Paul, alisema, chanzo cha ajali hiyo ni dereva kwenda mwendo kasi kuelekea Kaliua.

Abiria mwingine aliyesafiri na familia yake katika basi hilo, Mathew Andrew, alisema dereva alianza na mwendo wa kasi na alielezwa kupunguza mwendo, lakini alikaidi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo juzi na kwamba watu watatu walifariki dunia na miili yao kuhifadhiwa chumba cha maiti Hospitali ya Wilaya Kahama.

Aliwataja majeruhi hao kuwa ni Doris Machibya (16), Masoud Juma (35) na Halima Masolwa (50)



Mabaki ya gari aina ya Fuso lenye namba za usajili T380DVF lililokuwa limebeba mchele likitokea Tabora kwenda Moshi, mkoani Kilimanjaro, baada ya kugongana na basi kampuni ya Mohamed Classic lenye namba T643, linalofanya safari zake kutoka Arusha kwenda Kigoma, katika Kijiji cha Ming'enyi, kata ya Gehandu wilayani Hanang', mkoani Manyara jana na kusababisha vifo vya watu watatu akiwemo dereva wa fuso hilo, Filbeth Mrema (29) na wasaidizi wake wawili. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Diwani aliyetoweka miezi mitatu apatikana

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limefanikiwa kumpata Diwani wa Kawe, Mutta Rwakatare, baada ya kumfuatilia na kumkuta akiwa kwenye nyumba ya mwanamke Ashura Ally, mkazi wa Tabata Darajani jijini.

Siku chache zilizopita, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, alitangaza kutoonekana kwa diwani huyo nyumbani kwake, ofisini na jimboni tangu mwezi Februari mwaka huu bila kupatiwa taarifa yoyote ya udhuru.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema jana kuwa walimpata Diwani Rwakatare Mei 23 mwaka huu na baada ya kumhoji Ashura ambaye alikutwa akiwa na diwani huyo nyumbani kwake, alidai kwamba Rwakatare ni rafiki yake wa siku nyingi na urafiki wao upo kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Kamanda Muliro alisema mwanamke huyo alifafanua kwamba Diwani Rwakatare alifika nyumbani kwake Mei 19 mwaka huu akiwa katika hali ya ulevi uliopindukia.

"Kutokana na mazingira ya ulevi ambayo diwani huyo alikutwa nayo na maombi yaliyotolewa na ndugu zake kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya matibabu, ndugu pia walitoa kumbukumbu za nyuma, mwenendo na tabia zake, hivyo Jeshi la Polisi limemkabidhi kwa ndugu zake kwa matibabu na tiba zaidi ya kisaikolojia," alisema.

Kamanda Muliro alitoa wito wa wananchi na wanafamilia kuwa makini na tabia na mienendo ya ndugu, jamaa na marafiki na pindi wanapokuwa hawaonekani, watoe ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika hatua za kuwatafuata.

Mmoja wa wakazi wa kata ya hiyo, Juma Bakari, alitoa maoni yake kuhusu kilichotokea dhidi ya diwani wake, alidai kuwa jambo alilolifanya Rwakatare halileti tafsiri nzuri kwa familia yake na jamii inayomzunguka.

Alisema kiongozi aliyeaminiwa na watu na kupewa nafasi ya kuwaongoza, kuwasemea na kuwawakilisha katika nyanja mbalimbali zinazohusiana na masuala ya kijamii, anapokwenda kinyume cha maadili ni kama anawaangusha na kutowatendea haki wale waliompatia nafasi ya uongozi.

"Ukiwa kiongozi wa umma unapaswa kutambua kuwa wewe ni kiyoo cha jamii, hivyo ni muhimu kuwa na umakini wa hali ya juu na miendendo yako na kila jambo unalolifanya huku ukijua kuwa kuna watu wengi wako nyuma yako wanakutazama," alishauri Bakari.

## Nape awaagiza Ma-RC uhakiki anwani makazi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amewataka wakuu wa mikoa kufanya uhakiki wa takwimu za operesheni ya anwani za makazi kwenye maeneo yao hususan usimikaji wa miundombinu ya nguzo zenye majina ya barabara na mitaa pamoja na namba za nyumba.

Akizungumza katika kikao kazi na wakuu hao jijini hapa jana, Waziri Nape, alisema hali hiyo imetokana na takwimu za usimikaji wa miundombinu hiyo kuonyesha zipo chini ikilinganisha na uhalisia wa kilichotekelezeka katika mikoa.

"Ukiangalia hali ya takwimu kwa mfano Mkoa wa Lindi inaonekana ni asilimia mbili tu ya physical signs ndiyo imetekelezwa, lakini uhalisia haupo hivyo kwa kuwa nimepita mikoa mingi hadi Zanzibar nimejionea, lakini bado takwimu zinaleta utata hivyo niwaombeni sana twendeni tukahakiki ili sisi na nyie tuzungumze lugha moja kwa kupata takwimu halisi," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliwataka wakuu wa mikoa kusimamia kanuni za utekelezaji wa anwani za makazi ambazo ndio msingi wa utekelezaji wa zoezi hilo ikiwa ni pamoja na kuwabana watendaji kutumia fedha za mapato ya ndani bila kuathiri wala kutumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi mingine ya maendeleo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonaz, alisema kuwa zoezi la utambuzi wa makazi ya watu ni moja ya eneo muhimu litakalosaidia nchi kuingia kwenye uchumi wa kidijitali ambao hauna mipaka na unaoruhusu wananchi kujihusisha na shughuli za kiuchumi mahali walipo.

"Niwashukuru sana wakuu wa mikoa kwa kufanya kazi hii kwa kiwango cha juu na ufanisi mkubwa ambapo sasa tumefikia asilimia 106.62 ya utambuzi wa makazi ambapo asilimia hizi zimedhihirisha kuna makazi tuliyokuwa hatuyatambui awali na kupitia zoezi hili tumeyatambua na yatajumuishwa kwenye mipango ya maendeleo," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Majaliwa amsimamisha Mkurugenzi Halmashauri

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemsimamisha kazi Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Dk. John Pima, kwa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Mbali na mkurugenzi, watumishi wengine waliosimamishwa ni Mweka Hazina wa Jiji, Miriam Shasheni, Joel Mpango (ofisa ununuzi), Alex Telehema, Nuru Sakwale wa idara ya mipango na John Maduhu.

Waziri Mkuu aliwasimamisha kazi watumishi hao jana jijini hapa wakati akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Baada ya kuwasimamisha kazi watumishi hao, alimwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuanza kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo mara moja.

"Kwa mujibu wa sheria, natangaza kumsimamisha Dk. Pima, Mariamu, Innocent, Alex, Nuru na Joel kupisha uchunguzi ufanyike na CAG, TAKUKURU na TAMISEMI ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). Nikitoka hapa kazi hiyo ianze mara moja na ninaahidi hakuna mtu atakayeonewa kama hajafanya kosa lolote," alisema Majaliwa.

Alisema ni muda mrefu halmashauri hiyo inadaiwa madeni makubwa na imeshindwa kuyalipa ilhali inakusanya mapato mengi ya ndani.

"Halmashauri ya Jiji la Arusha, inadaiwa madeni makubwa na mmeshindwa kulipa wazabuni mfano kampuni ya Cherry General ICT, wanadai Sh. milioni 472, na halmashauri mlikuwa na Sh. bilioni moja na serikali iliwapatia Sh. milioni 500 kwa ajili ya kujenga masoko ya machinga lakini kampuni hii iliyopewa tenda ya kupeleka malighafi kwa nini hamkulipa fedha zake?" Alihoji Waziri Mkuu.

Kadhalika, Waziri Mkuu alionyesha kuchukizwa na kitendo cha mkurugenzi huyo kuhamisha watumishi ovyo kwa kuwa tangu Januari, mwaka huu, halmashauri imehamisha watumishi 50 kitu ambacho si cha kawaida.

"Halmashauri hii imeweka rekodi. Tangu Januari hadi sasa jumla ya watumishi 50 wamehamishwa kitu ambacho si cha kawaida kutokea," alisema Majaliwa.

Pia alisema uhusiano mbaya kati ya watumishi katika jiji hilo, imekuwa moja ya sababu ya ucheleweshaji wa maendeleo kwa kuwa kumekuwapo na makundi mbalimbali.

"Napenda kusisitiza katika Jiji la Arusha kwa viongozi walioko kumekuwapo na uhusiano ambao kati yao na imekuwa moja ya sababu ya kuchelewesha maendeleo," alisisitiza.


**Air Tanzania**
*The Wings of Kilimanjaro*

## EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is implementing its five years Corporate Strategic Plan (2017/2018-2020-2022) which includes the network expansion in local, regional and international destinations as well as improvement internal capacity by filling the vacancies as per approved organization structure. Applications therefore invited from **qualified Tanzanians to fill the position of Financial Accounting Manager** in the Directorate of Finance

**1. POSITION: Financial Accounting Manager**
**2. REPORTING TO: Director of Finance**

**3. QUALIFICATIONS:**
- Holder of Master Degree in one of the following fields: Accountancy, Finance, Commerce or Business Administration majoring in Accountancy or related qualifications from recognized institutions.
- Must have either CPA (T), ACCA, ACA, CIMA or related professional qualifications recognized by NBAA and preferably registered as "Associate Accountant" or "Fellow Accountant".
- Must have at least eight (8) years of working experience in Aviation Revenue Accounting and must be in Senior position.
- Must have IATA Certifications including but not limited to Fares and Ticketing, Passenger and Cargo Proration, Interline Accounting and Control –Pax & Cargo) and Sales Accounting & Control
- Must be knowledgeable of accounting applications.

**4. COMPETENCES**
- Excellent analysis and report writing skills
- Strong interpersonal, communication and presentation skills
- Ability to manage, guide and lead subordinates
- Attention to details
- Problem-solving and flexibility
- Strong ethical standards
- Excellent decision-making skills

**5. DUTIES AND RESPONSIBILITIES.**
The holder of the position will perform the following duties and responsibilities: -
- Owner of all accounting Standard Operational Policies (SOP) related to Aviation Revenue Accounting and shall maintain and update these in-line with existing financial regulation, Finance Act and IATA revenue accounting manual.
- Coordinate preparation of daily, weekly, monthly and quarterly revenue accounting reports to meet business needs and supporting business decisions.
- Overseeing and ensuring ICH billings is reconciled on each billing cycle to ensure accuracy, validity and completeness of invoices from business partners.
- Participate in pricing and fare committees by availing sales and business analysis at point of sales level, route level and Corporate business performance.
- Participate in budget committee in preparations of forecasted revenue by considering market parameters.
- Preparation of forecasted cash inflows from all company's revenue streams on quarterly and annually basis.
- Develop and maintain strong relationships with all key stake holders both internally and externally to ensure smooth business continuity.
- Manage BSP sales by ensuring proper sales accounting, Collection and reporting.
- Develop and build capacity for revenue accounting team skills through in house trainings.
- Develop, implement and maintain revenue accounting process, systems and internal controls to ensure efficiency and effectiveness.
- Implement and maintain aviation industry regulations, bilateral agreements and alliance with business partners related to revenue accounting & management.
- Ensure quality control of processed revenue Accounting and reference data maintenance to ensure continuous improvement.
- Ensuring compliance on new updates and publications related to revenue accounting management issued by IATA.
- Develop and implement Standard Operating Procedures (SOP) for managing and authorizing passengers' refunds.
- Responsible for month-end closing processes to include reconciling various G/L accounts, reviewing journal entries and preparing financial reports, for both internal and external reporting purposes.
- Demonstrate a strong understanding of end-to-end processes in all areas of Revenue Accounting aspects by providing reliable solutions and responses.
- Provide support to internal and external Auditors in all assignments related to revenue Accounting.

**6. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS**
Interested applicants must submit **a dully signed letter** for consideration of the application attached with the following: -
i. A detailed curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school), other relevant certificates, **Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)**
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of facts and/or qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**7. CLOSING DATES:**

Applicants should consider the following closing dates for each post as follows:

**Within Fourteen (14) days from the first date of this announcement**

The application letters should be directed to the following address: - Managing Director and CEO,

**Air Tanzania Company Limited,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM**
**Date of issue 24.05.2022**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha miundombinu sio cha kupuuza

**JUZI** wabunge wawili waliamua kuonyesha hisia zao kwa kufanya vitendo vitakavyogusa mioyo ya waandaaji wa makadirio ya bajeti, umma na wawakilishi wenzao kuona maeneo hayo kwa jicho la tofauti.

Wabunge hao walikuwa wakichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2022/23, ambayo kila aliyesimama alipaza sauti ya barabara yake kutojengwa au imekwama au ilikuwa ni ahadi ya mkuu wa nchi na imesahaulika. Wabunge hao ni Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay ambaye aliomba kupiga sarakasi na kabla hajaruhusiwa na Spika Dk. Tulia Ackson, akawa ameshatekeleza alichokidhamiria.

Mwaka jana wakati wa bajeti hiyo hiyo tena aliongea kuhusu ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Mbulu Haydom, aliuomba Spika amruhusu aruke sarakasi kutoka alipokuwa amekaa kushoto mwa Spika hadi mbele, lakini alimsihi asifanye hivyo, alitii na kutoa mchango wake huku akitishia kushika Shilingi ya mshahara wa waziri ili bajeti isipite.

Mbunge mwingine ni Jerry Silaa wa Jimbo la Ukonga, alilia kwa uchungu kwa kuwa mkandarasi aliyepewa ujenzi wa mwendokasi ndiye aliyeboronga eneo jingine, jambo linaloumiza sana. Kimsingi wabunge hawa hawajafanya hivi labda kutafuta sifa kwa umma au mamlaka, wametafuta namna yao ya kufikisha hisia zao ili kutaka uwajibikaji, huenda na wengine walio na ahadi za tangu enzi za Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, wangetamani kufanya jambo.

Ukifuatilia vikao vya Bunge wakati wa maswali na majibu mengi yamejikita kwenye afya, maji, barabara na elimu, hulalamika kwamba wameachwa nyuma kwenye ujenzi wa miundombinu muhimu.

Kutokana na kilio cha wabunge, Spika mara kadhaa ameitaka serikali kuja na mkakati wa kutatua kero hizo, kwamba waangalie mgawanyo wa bajeti hizo na hasa ahadi za viongozi ambazo ni za muda mrefu, huku akieleza kuna barabara lazima mbunge asimame kuuliza swali la nyongeza au achangie mjadala. Kimsingi jitihada zimefanyika za kuunganisha mikoa, sasa imebaki kuunganisha wilaya na wilaya, pia kufika kwenye mitaa.

Ni lazima wanaoandaa bajeti kuangalia malalamiko ya wabunge, kwa kuwa keki ya taifa inapaswa kumfikia kila Mtanzania, isiwe kuna eneo fulani limetengewa fedha nyingi, lakini inapoibuka hoja ya mkandarasi kujenga chini ya kiwango isiachwe ikapotea hewani bali ifanyiwe kazi ili kuepuka hasara.

Mathalani, wananchi tunajiuliza barabara ya Mwenge Tegeta ya njia nne haina miaka 10 tangu imejengwa ila imekuwa ikifumuliwa na kuwekewa tabaka jipya la lami, yote hiyo ni fedha, lakini swali linakuwa ni kwanini inatengenezwa kwa viwango vya muda mfupi?


Uandaaji wa bajeti huanzia kwenye Kamati za Maendeleo ya Kata (WDC), ambayo Diwani wa kata husika ndiye mwenyekiti, baadaye Baraza la Madiwani ambalo huongozwa na Mwenyekiti wa halmashauri, baadaye Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na kwenda Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na baadaye wizara.

Maana yake bajeti ni shirikishi na humo vipaumbele huchujwa kulingana na umuhimu wake kwa taifa, na kama kuna barabara imetoka Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na kuwa chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), ili kuwezesha utekelezaji.

Barabara nyingi zinazolalamikiwa ni zilizopo chini ya TANROADS, maana yake lazima kuja na mkakati wa kuhakikisha zinakamilika, kwa kuwa mbunge ana haki ya kufanya 'kituko' ndani ya muhimili wa kutumga sheria kwa kuwa ahadi yake ni ya miaka mingi, anaona fedha zimetengwa ghafla zimeenda kulipa madeni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanasiasa yapokeeni maridhiano yanayohimizwa

**MAKAMU** Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, amekuwa akichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuimarisha demokrasia ndani ya vyama vya siasa tangu achaguliwe kushika nafasi hiyo.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kuwataka viongozi na wanachama wa CCM kuwa tayari kwa maridhiano ya kisiasa aliyoyaanzisha Rais Samia Suluhu Hassan kati ya chama hicho tawala na vyama vyote vya siasa.

Kinana ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM ni Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, anaonyesha mfano wa kuigwa kwa kuanzisha mchakato huo kwa kukutana na vyama na taasisi mbalimbali za kisiasa.

Anataja mambo manne anayoshughulikia kuwa ni maridhiano, kuvumiliana, mabadiliko kwenye taasisi na kulijenga upya taifa, kwa kuwa Tanzania ni ya vyama vingi vya siasa, hivyo kuwapo kwa maridhiano ni jambo muhimu.

Ni kweli kwamba, siasa si uadui, tena kuna maisha baada ya siasa, hivyo ni wazi hakuna sababu ya msingi ya kugombana wenyewe kwa wenyewe kama vyama au kugombana na chama tawala na kusababisha kutoelewana.

Hatua zinazohimizwa na Kinana, zinaakisi kile ambacho Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, alikianzisha kwa lengo la maridhiano kati ya CCM na vyama vyote vya siasa.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba, mazungumzo ya wanasiasa yanajenga maridhiano yatakayoweka mazingira bora na wezeshi ya kuendeleza amani na utulivu kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wake.

Kwa ujumla ni kwamba, mazungumzo ya pamoja yanafungua ukurasa mpya wa siasa nchini, yangekuwa ni malengo ya kila mwanasiasa ili kuzaa matunda, kwa kuwa na siasa za kupingana kwa hoja na kuisimamia serikali na raia kuwa na Tanzania inayosonga mbele.

> **Lakini, pia ingekuwa ni vyema kama Baraza la Vyama vya Siasa linatimiza wajibu wake inavyotakiwa, ikiwamo kumshauri Msajili wa Vyama vya Siasa juu ya migogoro inayotokea katika vyama vya upinzani.**

Lakini, pia ni vyema kukumbusha wanasiasa kuwa kuna maisha baada ya siasa, hivyo si vyema kuchukiana kwa sababu ya siasa, na ingependeza kama fikra hizo zitatupwa mbali na kuacha maridhiano yachukue nafasi.

Pamoja na hayo, uadui katika siasa ungebaki katika majukwaa ya kinadharia lakini baada ya hapo wanasiasa wabaki kuwa wamoja, wanaojadiliana kuhusu maendeleo na mustakabali wa Tanzania bila kujali itikadi za vyama vyao.

Ikumbukwe kuwa Rais Samia amekuwa akisisitiza kila mara kuwa Tanzania haitajengwa na chama kimoja, na kwamba ni lazima kuwe na ushirikiano, na kuwataka Watanzania wote kushiriki kujenga nchi yao kwa misingi iliyo sawa.

Mbali na hilo, anagusia kuwa vyama vya siasa vinao umuhimu mkubwa katika kuangalia na kukosoa yale yanayoendelea katika serikali na kutoa maoni ili kuirekebisha serikali iliyoko madarakani. Katika mazingira hayo, ni wazi kwamba yapo matumaini ya baadaye ya uwapo wa siasa na demokrasia inayoshamiri ambayo Rais anaamini kuwa ndiyo ambayo Watanzania wanaitaka na kuitamani.

Lakini, pia ingekuwa ni vyema kama Baraza la Vyama vya Siasa linatimiza wajibu wake inavyotakiwa, ikiwamo kumshauri Msajili wa Vyama vya Siasa juu ya migogoro inayotokea katika vyama vya upinzani.

Kumshauri Msajili wa Vyama vya Siasa juu ya masuala yenye maslahi kwa taifa kuhusiana na vyama vya siasa au kuhusiana na hali ya kisiasa nchini ili kuhakikisha zinapotokea tofauti, maridhiano yachukue nafasi.

Lina jukumu la kumshauri kwani Baraza la Vyama vya Siasa linaundwa ndani ya Ofisi ya Msajili na wajumbe wake wakijumuisha viongozi wa kitaifa wawili wa kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu.

# TAKUKURU yaonya matapeli wa ardhi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani, imewaonya watu wanaodaiwa kuhusika kwenye migogoro ya ardhi kwa kuuza maeneo holela.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, Christopher Myava, alipokuwa akitoa taarifa ya utendaji kazi ya taasisi hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema kuna watu wanatuhumiwa kuuza eneo kwa mtu zaidi ya mmoja jambo ambalo limekuwa chanzo cha kutoisha kwa migogoro ya ardhi katika mkoa.

Myava alisema taasisi hiyo iko kazini kupambana na watu hao wanaodaiwa kushiriki kufanya utapeli ili wasiwaingize wawekezaji wenye lengo la kupata maeneo katika mkoa na kuzorotesha uwekezaji.

Alisema kati ya malalamiko yaliyopokewa katika kipindi hicho, 17 yanahusiana na migogoro ya ardhi ambayo inachangiwa na watu wanaodaiwa kuwa matapeli.

Myava alisema malalamiko 98 yalipokewa katika kipindi cha miezi mitatu, 51 yalihusu rushwa ambayo yalianzishiwa majalada ya uchunguzi huku malalamiko 47 yakielezwa kuwa hayakuhusu rushwa.

Mkuu huyo pia amewatahadharisha wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujiepusha kujihusisha na rushwa.

"Nawaambia TAKUKURU hatujalala tuko kazini. Tutazuia vitendo vyote vyenye viashiria vya rushwa na kwa matapeli wa ardhi tunaendelea kuchunguza malalamiko yaliyoletwa kukomesha tabia hii isituchafulie mkoa wetu" alisema .

Katika kipindi cha miezi mitatu, TAKUKURU imeeleza kuwa imefuatilia miradi 182 katika sekta za afya, elimu, ujenzi na maji yenye thamani ya Sh. Bilioni 8.4.

# Tanzania, Marekani zasherehekea miaka 5 mradi mboga na matunda

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI kutoka Serikali ya Marekani na Tanzania wamesherehekea mafanikio ya mradi wa mboga na matunda uliotekelezwa na Mpango wa Feed the Future kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Kupitia ushirikiano na Serikali ya Tanzania, mradi huo wa miaka mitano uligharimu Dola za Marekani milioni 25 (sawa Sh. 58,139,534,884) na umeboresha hali ya lishe kwa mamia na maelfu ya Watanzania katika mikoa mitano nchini kote.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo ya kuhitimisha utekelezaji wa mradi wa mboga na matunda akiambatana na Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, Kate Somvongsiri.

Mkurugenzi Somvongsiri alisema, sekta ya kilimo Tanzania ambayo inachangia theluthi moja ya Pato la Taifa na kuajiri asilimia 75 ya watu wote ni muhimu katika kufikia ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.

Katika kipindi cha miaka mitano iliopita, mradi wa Feed the Future Mboga na Matunda ulishirikiana na Serikali ya Tanzania kuboresha mbinu za uzalishaji na umwagiliaji; na kuongeza upatikanaji wa mbegu na kuboresha lishe kwa zaidi ya wanufaika 874,000, asilimia 58 kati yao wakiwa vijana.

Mradi huo pia ulipanua mtandao wa soko la mazao ya kilimo; na kuimarisha ukuaji wa kilimo cha mboga na matunda.

Taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa Marekani ilisema matokeo ya moja kwa moja ya afua za mradi huo ni pamoja na kuongeza uwekezaji wa biashara ndogo na za kati kwenye kilimo cha mboga na matunda kwa zaidi ya Dola za Marekani milioni 154 zilizozalisha bidhaa na huduma zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 373.



Ndugu, jamaa na marafiki wakiuzika mwili wa kijana Hamisi Mayunga (19) mkazi wa kijiji cha Dulisi Kata ya Sekebugolo wilayani Kishapu, aliyedaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi kifuani na mlinzi Emmanuel Chacha wa Kampuni ya Sam Security, walipokuwa wakivua samaki na wenzake wanne kwenye bwawa lililopo ndani ya mgodi wa madini ya almasi wa El-Hilali, wilayani Kishapu Mei 20, mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vilio, simanzi vyatawala mazishi ya kijana aliyeuawa kwa risasi mgodini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VILIO na simanzi vilitawala jana katika kijiji cha Dulisi, Kishapu mkoani Shinyanga, wakati wa mazishi ya Hamisi Mayunga aliyeuawa kwa kupigwa risasi ndani ya mgodi wa almasi wa El- Hilal.

Wakati hali ikiwa hivyo, wananchi wa kijiji hicho na vya jirani waliohudhuria maziko hayo, walilaani tukio hilo lililofanywa na mlinzi wa kampuni ya Sam Security, Emmanuel Chacha.

Tukio hilo la mauaji lilitokea Mei 20, mwaka huu, wakati Mayunga akiwa na wenzake wanne pamoja na kaka yake, Robert Mayunga (21), wakivua samaki katika bwawa lililoko ndani ya mgodi huo ndipo walipokamatwa na walinzi na kusababisha mauaji.

Diwani wa Sekebugolo, Ferdinand Mpogomi, akizungumza jana wakati wa mazishi ya kijana huyo nyumbani kwao, kijiji cha Dulisi, alisema wanalaani tukio hilo pamoja na mauaji ya vijana wengine.

Alisema wananchi wa Sekebugolo kwa ujumla, wamelaani matukio ya vijana kuendelea kuuawa ndani ya migodi inayozunguka wananchi wilayani humo, likiwamo na la kijana Mayunga.

"Kifo cha kijana huyu kimetusikitisha sana ndiyo maana mmeona watu wamelia na kuzirai. Hamisi alikuwa kijana mdogo sana hakustahili kufa kikatili namna hii," alisema Mpogomi.

"Nawapongeza wananchi kwa kuwa wavumilivu na kitusikiliza sisi viongozi kwa sababu mngeweza kuandamana na kufanya fujo kwenye mgodi lakini suala hili tumeviachia vyombo vya dola vinalifanyia kazi," aliongeza.

Naye kaka wa marehemu, Robert Mayunga, ambaye walikuwa naye kwenye mgodi huo, alisema waliingia saa 1:00 jioni kuvua samaki wakiwa wanne na walipotega samaki walikwenda kulala vichakani wakisubiri samaki wanase ndipo wakakamatwa.

Alisema walikamatwa na walinzi wa kampuni hiyo ya Sam Security saa 6:00 usiku na walipoanza kukimbia ndipo mdogo wake akapigwa risasi na kufariki dunia.

Kwa mujibu wa kaka huyo wa marehemu, wakati mdogo wake akipigwa risasi, yeye alikwenda kujificha ndani ya maji kwenye bwawa ambalo walikuwa wakivua samaki na baada ya walinzi kuondoka, ndipo alitoka na kukimbilia nyumbani.

"Sisi huwa tunaingia mara kwa mara ndani ya mgodi huo kuvua samaki. Si mara ya kwanza na baadhi ya walinzi wanatufahamu lakini siku hiyo sijui ilikuaje tu na kuamua kuturushia risasi na kumuua mdogo wangu," alisema.

Baba mzazi wa kijana huyo, Mayunga Inegele, aliiomba serikali kutenda haki juu ya kifo cha mtoto wake kwa kumkamata mlinzi aliyemuua na kumchukulia hatua kali za kisheria.

Alisema hata kama mtoto wake ametenda kosa kuingia ndani ya mgodi huo, hakupaswa kupigwa risasi bali angekamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Alibainisha kwamba kilichofanyika ni ukiukaji wa haki za binadamu.

Naye mtetezi wa haki za binadamu, John Myola kutoka Shirika la AGAPE, aliiomba serikali kuingilia kati ikiwamo kuunda tume kuchunguza kukithiri mauaji ndani ya mgodi wa El - Hilal.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea mauaji hayo na kubainisha kuwa wanamsaka Chacha ambaye alikimbia baada ya mauaji hayo.

Alisema pia wanawashikilia walinzi wenzake wanne kwa ajili ya upelelezi zaidi na kuonya walinzi wa kampuni kutumia silaha holela na kusababisha mauaji.

Tukio hilo ni la pili kutokea ndani ya mgodi huo wa El - Hilal likiwahusisha walinzi wa kampuni binafsi. Tukio la kwanza lilitokea Machi 10, mwaka huu, baada ya Cosmas Hamisi (25) kutoka kijiji cha Mwang'olo, naye kuuawa kwa kupigwa risasi.

# Waziri Mabula asisitiza ushirikiano na wanahabari

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka waandishi wa habari kutumia nafasi zao vizuri kama jicho la serikali katika kutoa elimu na ufahamu kwa wananchi kuhusu sekta ya ardhi.

Pia amewataka kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha migogoro ya ardhi inapungua kwa asilimia 100 kama si kutokuwapo kabisa katika jamii.

Kauli ya Waziri inakuja huku kukiwa na taarifa za upotoshaji zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kueleza kuwa migogoro ya ardhi imeanza kushamiri upya.

Dk Mabula alisema hayo juzi wakati wa mkutano wa majadiliano ya kisekta kati ya wizara na wadau wa sekta ya ardhi uliofanyika jijini Dar es Salaam.

"Ofisi zipo wazi pale mtakapotaka ufafanuzi wa sera, sheria, kanuni na miongozo ya ardhi tushirikiane katika kutoa elimu ili kutokomeza migogoro ya ardhi," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, wizara yake iko tayari muda wowote kupokea na kuchakata mapendekezo yanayoweza kuendelea kuleta mapinduzi katika sekta ya ardhi nchini.

"Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za utatuzi wa changamoto za sekta ya ardhi ikiwamo kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za ardhi, kuendelea kuimarisha na kuziwezesha ofisi za ardhi za mikoa katika kuhakikisha huduma zinapatikana karibu na wananchi," alisema.

Aidha, katika juhudi za kurahisisha utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa wananchi, alisema wizara imeanzisha kituo cha Mwasiliano kwa Wateja ambapo wananchi wanaweza kuwasilisha malalamiko yao kwa njia ya simu na kutafutiwa ufumbuzi bila kufika ofisi za ardhi. "Sekta ya ardhi ni moja ya nguzo muhimu ya kuwezesha kuleta maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla na utekelezaji wa majukumu ya sekta hiyo utawezesha shughuli mbalimbali za sekta zingine na kukuza uchumi wa kipato cha kati kupitia uwekezaji katika ardhi," aliongeza.

Pia alisema serikali imeendelea kufanya maboresho kwenye sekta ya ardhi kwa kutunga na kusimamia sera na sheria mbalimbali sambamba kuandaa kanuni, miongozo na kuratibu utekelezaji wa mikakati mbalimbali ndani ya sekta kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa milki salama za ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Aidha, Waziri Mabula alisema sekta ya ardhi imeendelea kuwa kiungo wezeshi kwa sekta zingine za uzalishaji zikiwamo viwanda, kilimo, mifugo na miundombinu.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akikata keki kuzindua Bodi ya Magavana ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Kijitonyama mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Amon Mpanju, Katibu Mkuu wa wizara hiyo Zainab Chaula (wa pili kulia), Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Sophia Simba (wa pili kushoto) na Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Joyce Nyoni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wanaodaiwa kuiba fedha hekalu wasomewa mashtaka upya

**Na Grace Gurisha**

WASHTAKIWA watatu wanaotuhumiwa kuiba zaidi ya Sh. milioni 400 mali ya Hekalu la Shee Sanatan Dharma Sabha, wamesomewa upya mashtaka yao matatu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Washtakiwa hao ni Akshary Motichand, Vasant Solanki na Ramesh Shah, ambao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Isaya wa Mahakama hiyo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai katika tarehe zisizofahamika kati ya Januari hadi Novemba mwaka 2016, jijini Dar es Salaam washtakiwa hao walikula njama ya kutenda kosa la wizi.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kwamba, katika tarehe na eneo hilo, mshtakiwa Motichand aliiba Sh. 438,808,643 mali ya Hekalu la Shee Sanatan Dharma Sabha.

Katika shtaka la tatu, Wakili Mwanga alidai katika tarehe hizo mshtakiwa Shah aliiba Sh. milioni 20.7 mali ya hekalu hilo.

Baada ya kusomewa mashtaka yao, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na walikuwa tayari kuwasomea maelezo ya awali.

Hata hivyo, upande wa utetezi uliomba wapangiwe tarehe nyingine kwa sababu mmoja wa mawakili ana udhuru.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Mei 31, mwaka huu kwa ajili ya washtakiwa hao kusomewa maelezo ya awali.

## Askari TZ kushiriki mafunzo Uganda

**Na Richard Makore,** MWANZA

KIKOSI cha askari wa ulinzi na usalama kinatarajia kuondoka nchini kwa ajili ya kushiriki mafunzo maalum yanayohusisha nchi sita za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambayo yatafanyika Uganda kuanzia Mei 28 hadi Juni 10, mwaka huu.

Wapiganaji hao pamoja na raia jana walikabidhiwa bendera ya taifa na Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali Antony Sibiti katika kikosi cha usafirishaji cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kilichoko Nyegezi, jijini Mwanza.

Akizungumza na askari hao, Meja Jenerali Sibiti alisema kikosi hicho kitaondoka nchini Mei 28, kuelekea nchini Uganda na kitakaa kwa siku 14.

Alisema wanajeshi wa JWTZ watakuwa 240, Polisi 47 na wengine wakiwamo Uhamiaji, Magereza, Zimamoto, Usalama wa Taifa pamoja na raia jumla 13.

Alisema lengo la mafunzo hayo ambayo yanajulikana kama ushirikiano imara, yanalenga kupata mbinu za kupambana na ugaidi katika nchi wanachama wa EAC, kusaidia nchi inayokumbwa na machafuko ya kisiasa, kupata mbinu za kukabiliana na maafa pamoja na uharamia.

Aliwataka askari hao pamoja na raia kudumisha umoja na mshikamano katika kipindi chote cha mafunzo watakapokuwa nchini Uganda.

Aliwataka kujifunza mambo mazuri katika nchi hizo na kwamba nchi imewaamini na wao wahakikishe wanaleta picha nzuri kwa taifa.

Kwa upande wake, Mkuu wa msafara huo, Brigedia Jenerali, Charles Ndiege, akizungumza jana katika kikosi hicho, aliwataka askari hao kuhakikisha wanajifunza mambo mazuri na kuyaelewa kwa faida ya taifa.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu na kwamba yalianza kufanyika kwa mzunguko tangu EAC ilipoanzishwa kwa mara ya pili baada ya mwaka 1977 kuvunjika.

Aliwataka kutumia uwezo wao wote kujifunza na kushirikiana na wenzao kutoka nchi hizo za EAC ambao wanashiriki mafunzo hayo.

**Kwa upande wake, Mkuu wa msafara huo, Brigedia Jenerali, Charles Ndiege, akizungumza jana katika kikosi hicho, aliwataka askari hao kuhakikisha wanajifunza mambo mazuri na kuyaelewa kwa faida ya taifa.**

## Watakaookwamisha ugawaji pembejeo kukiona

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SERIKALI wilayani Masasi mkoani Mtwara imewaonya watakaokwamisha au kuhujumu ugawaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima na kusababisha kutopatiwa pembejeo hizo za bure watachukuliwa hatua kali ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alipokuwa akizungumza na watendaji wa kata, mitaa, vijiji na madiwani kwenye kikao maalumu cha kupeana msisitizo wa majukumu ya ugawaji pembejeo hizo kwa msimu wa 2022/2023.

Kitta alisema Wilaya ya Masasi hadi sasa imepokea pembejeo za kilimo kwa ajili ya kugawa kwa wakulima, mifuko ya Sulpher 6,500 na dawa za maji za mbu wa mikorosho lita 20,929 na dawa za maji blatini na ubwiririunga 50,320 ambazo zote zitapelekwa kwa wakulima.

Alisema Rais Samia Suluhu na serikali yake imetangaza kutoa pembejeo za kilimo bure kwa wakulima wa korosho nchini na hakuna mkulima atakayeuziwa pembejeo hizo na kuwataka wakuu wa mikao na wilaya wahakikishe wakulima wapatiwa pembejeo hizo bure.

Kitta alisema Serikali ya Wilaya ya Masasi itahakikisha kila mkulima atakayekuwa na sifa ya kupewa ya pembejeo anapata kulingana na mgao utakavyokuwa na yeyote atakayehujumu zoezi la ugawaji na kusababisha wakulima kwenye eneo lake kutopata pembejeo atawajibika.

"Tukazigawe hizi pembejeo kwa wakulima kwa uadilifu na uaminifu, asitokee yeyote wa kuhujumu au kuiba sisi kama serikali hatutamfumbia macho tutamchukulia hatua kwa sababu atafanya wakulima wasipate pembejeo zao ambazo zinatolewa na serikali yao bure," alisema Kitta.

Alisema kuwa anawataka wajumbe wa kamati za pembejeo za kata na kijiji kuwa waaminifu na waadilifu katika kugawa pembejeo hizo kwa kufuata muongozo uliotolewa na serikali katika kugawa pembejeo hizo. Vile vile, alisema lengo la serikali kuamua kutoa pembejeo hizo bure kwa mkulima ni kuona uzalishaji wa korosho unaongezeka na kumfanya mkulima aweze kupata tija katika mazao.

Aliwataka wakulima ambao mashamba yao yalikuwa yamekufa kuanza kuyafufua na kuyasafisha, vilevile vijana kuacha kukaa vijiweni na kujikita katika kilimo ili kujiingizia kipato.

Haridi Chilungu, ameipongeza serikali kwa kuamua kutoa pembejeo hizo bure na wao kama wajumbe wa kamati za kata na vijiji wanakwenda kuzigawa kwa kuzingatia mwongozo wa serikali uliotolewa katika kugawa pembejeo hizo.

Shabani Kusenga, mjumbe wa kamati ya ugawaji pembejeo kijiji cha Mitonji, alisema wamejipanga kuhakikisha wakulima wa wanapata pembejeo za kilimo kwa wakati na bila changamoto yoyote.

# Transfoma 20,000 kununuliwa

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali inatarajia kununua transfoma mpya 20,000.

Alitoa kauli hiyo juzi katika maonyesho ya wizara yake yanayoendelea kwenye viwanja vya Bunge jijini hapa, yakizikutanisha taasisi zote zilizo chini ya wizara hiyo kwa lengo la kutoa fursa kwa wabunge kueleza matatizo yaliyopo majimboni ili yatatuliwe kwa pamoja.

Mbunge wa Morogoro Mashariki, Hamisi Taletale, alimwabia Waziri January kuwa jimboni kwake kata ambazo zina matatizo ya umeme ambako anahitaji wananchi wake wapelekewe huduma ni pamoja na Tomondo na Tegetero ambako pia kuna mradi wa serikali wa Sh. bilioni 24 wa Morong'anya na Kijiji cha Changa kinachohitaji transfoma.

Waziri January alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 utakaoanza baada ya siku 36 zijazo, transfoma mpya 20,000 zitanunuliwa na serikali.

**GHARAMA ZA UMEME**

Kuhusu gharama ya Sh. 27,000 katika kuunganishiwa umeme na matatizo yake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Felchesmi Mramba, alisema walikuwa na kikao cha kulitazama suala hilo na kuona linaathiri maeneo mengi nchini.

"Tumekubaliana na TANESCO (Shirika la Umeme) wameunda timu maalum ambayo itapitia maeneo yote ambayo hayajulikani ni vijiji lakini yapo mjini, wakishapitia na kuyaainisha tutayapa huduma za vijijini. Kwa hiyo, zoezi hili watalianza mara moja, bahati nzuri timu wameshaiandaa itazunguka kote," alisema. Waziri January, akizungumza maonyesho hayo, alisema wizara yake pamoja na taasisi zake zimekuwa zikigusa maisha ya wananchi moja kwa moja hasa umeme na mafuta.

"Kwa mara ya kwanza tumeamua kama wizara na taasisi zake kwamba hapa bungeni tufanye maonyesho ya siku tatu kuanzia leo (juzi), nina ofisi hapa, Naibu Waziri ana ofisi hapa na Katibu Mkuu ana ofisi hapa, Mkurugenzi wa TANESCO, REA (Wakala wa Nishati Vijijini), EWURA (Wakala wa Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji) tupo hapa kila mtu ana chumba chake.

"Pia tumegawanya mabanda kwa mikoa, mameneja wote wa mikoa na wilaya pamoja na makandarasi wa REA na wenyewe wapo hapa kila mkoa ili wabunge ambao wanawawakilisha wananchi yale maswali ambayo wanayo kuhusu wizara na taasisi zetu, huduma zinazotolewa wapate majibu hapa kwa wakati mmoja kwa haraka bila kuhangaika," alisema. Waziri Makamba alisema kama kuna mahali mkandarasi amechelewesha nguzo, waya au hajaonekana kupitia maonyesho hayo ataonekana.

"Na kwa sababu muda wa kuchangia bungeni ni mfupi na wengi hawawezi kutoa michango yao kwenye hotuba za bajeti na kuuliza maswali, hivyo tumeona wazipate kupitia maonyesho haya ili wapate majawabu na wawapelekee wananchi wao," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi REA, Julius Kalolo, alisema kila mwaka katika wiki kuelekea hotuba ya Wizara ya Nishati, wizara hiyo iliamua kuwe na maonyesho ya shughuli zinazofanyika.

Alisema wajibu wa REA ni kuhakikisha inapeleka nishati vijijini ambako kuna miradi ya muda mfupi ya miezi sita, tisa, ya mwaka, miezi 18 na miezi 24 kulingana na aina ya miradi yenyewe ilivyobuniwa na kuzinduliwa.

"Katika miradi mbalimbali kuna matatizo mbalimbali hujitokeza, moja wapo ni kuchelewa kumalizika kwa miradi au mazingira ambayo yanaathiri utendaji wa makandarasi ambapo yote huwa tunayazingatia.

"Kwa nini wengine wanachelewa au kusitishiwa mikataba yao? Ni kwa sababu tunazingatia mikataba iliyoingiwa kati ya REA na makandarasi huwa wazi na inatakiwa baada ya muda fulani awe amefikia lengo, tukiona hajafikia mikataba mingi inaruhusu mwajiri (REA) kutoa barua kwa mkandarasi ajieleze kwa nini ameshindwa kufikia hatua hiyo.

"Baada ya maelezo yake wataalamu wanafanya tathmini wanaweza kumpa onyo kutoa mapendekezo kwa uongozi na kuja kwenye bodi kwamba asitishiwe mkataba kwa sababu hakuna namna anaweza kumaliza kazi kwa muda uliwekwa au hata akiongezwa hawezi kukamilisha. Hii imetokea kwa makandarasi wawili na tuliwabadilisha tukaweka wengine," alifafanua.



Ofisa Huduma kwa Wateja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA), Juliana Saimon (wapili kulia), akiwahudumia wananchi wa Mtaa wa Mpiji-Magoe, wakati wa zoezi la utoaji elimu na uhamasishaji wa kuunganishiwa maji kutokana na utekelezaji wa mradi wa maji Machimbo-Kilongo katika dawati la huduma kwa wateja serikali ya mtaa huo, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kuwaibua wagonjwa wa TB

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WARATIBU wa Kifua Kikuu na Ukoma Kanda ya Ziwa, wametakiwa kuwaibua wagonjwa wa TB na kuwaanzishia matibabu ili wasiendelee kukimbilia kwa waganga wa jadi.

Uibuaji huo ni pamoja na utoaji wa elimu ya ugonjwa huo na dalili zake, kuwafuatilia baada ya kuwaanzishia matibabu na kwa mgonjwa atakayehudhuria vipindi vyote vya matibabu serikali itampatia Sh.100,000 kama sehemu ya usafiri na chakula lishe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Maalum Ngazi ya Taifa ya Tiba ya Magonjwa ya Ambukizi Kibong'oto, Dk. Leonard Subi, alibainisha hayo juzi wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma ngazi ya mikoa na wilaya za Kanda ya Ziwa kilichofanyika Manispaa ya Kahama.

Alisema, wagonjwa wengi wa TB wanashinda kwa waganga wa jadi kupata matibabu ya asili huku wakiamini wamerogwa jambo ambalo sio kweli na wanazidi kuwaambukiza wengine, waganga wa jadi hawana vipimo vyovyote vya kutambua mgonjwa mwenye TB sugu.

Dk. Subi alisema, zaidi ya asilimia 30 ya wagonjwa bado hawawapati na kuwasihi waratibu hao kuwa na uibuaji mzuri katika maeneo yao wanapotoka kwa kuwapatia elimu wananchi, wafahamu TB ni nini, dalili zake na kuwajuza serikali inagharimia matibabu yote ikiwamo dawa na uchunguzi bure.

Alisema, serikali imetoa mashine za kugundua mgonjwa wa kifua kikuu ndani ya saa mbili katika halmashauri zote nchini na vitu vyote vimepata mashine hizo tofauti na kipindi cha nyuma waligundua wagonjwa kwa muda wa siku mbili hadi tatu hali ambayo ilikuwa ikisababisha mgonjwa kuanza matibabu.

"Lazima mgonjwa wa kifua kikuu wakati wa matibabu yake tushirikiane na wanafamilia yake kuhakikisha anapata matibabu ipasavyo, zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa wa TB sugu wanapona hivyo dawa zetu zinafanyakazi vyema," alisema Dk. Subi.

"Nchi yetu imepiga hatua na imekuwa nchi bora inayofanya vizuri zaidi mwaka hadi mwaka kwenye matibabu ya wagonjwa wa TB na uzuri huu unaletwa na waratibu wetu waliopo ngazi za mikoa na wilaya hivyo elimu tunayokwenda kuitoa hapa iwe na tija kwenu."

Naye Ofisa Mtakwimu kutoka Wizara ya Afya, Yusto Erasto, alisema wagonjwa wa TB ni wengi, lakini wanaofika katika vituo vya afya kupata matibabu ni wachache na kwamba lazima kuwe na mikakati mizuri ya kuhakikisha wote wanafikiwa na kupata matibabu.

Alisema, kila mratibu wa ugonjwa huo anatakiwa kutumia mfumo wakati wa kumhamisha mgonjwa wake wa TB na sio kutumia mfumo wa makaratasi kama ilivyokuwa hapo awali na kuhakikisha anamfuatilia kujua hali yake ya matibabu inaendeleaje ili kukata mnyonyoro wa maambukizi ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake, Mratibu wa TB na ukoma kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Mageda Pastory alisema, wagonjwa wa maambukizi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi (HIV) wanazaa wagonjwa wa TB na lazima kuwafuatia katika maeneo yao kuwapatia elimu ya ugonjwa na dalili zake na kuwapatia matibabu.

Alisema, kila mmoja atakiwa kuwaibua na kufuatilia hali zao na hakuna haja ya kuwaacha wenye dalili za TB na huku inawekana kuanza matibabu yao mara moja na kwamba mgonjwa mwenye kifua kikuu sugu anapoanzishiwa dawa na kutumia ipasavyo anapona bila shida yoyote.

# Mafao ya wastaafu kulipwa kwa wakati

## • Uhakiki taarifa waja mkoa kwa mkoa

OFISI ya Waziri Mkuu inatarajia kuanza ziara ya mkoa kwa mkoa kwa ajili ya kusikiliza kero za wastaafu ikiwamo kuhakiki taarifa zao ili kulipwa mafao yao kwa wakati.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Singida Mashariki (CCM), Miraji Mtaturu.

Mbunge huyo alisema malalamiko makubwa ya kutopewa mafao yao kwa wakati yanatokana na waajiri kutowasilisha michango yao kwenye mifuko.

"Nini kauli ya serikali katika hili kwa kuwa limekuwa kero kubwa kwa wastaafu? Pia wamekuwa wakiombwa taarifa zao upya baada ya kustaafu, serikali ina taarifa zao kwa miaka 30. Je, haioni ni usumbufu kuwaomba taarifa ambazo wanazo miaka yote kwa umri wao?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema tayari yalishatolewa maelekezo mahsusi na waziri mwenye dhamana kuhusu ucheleweshaji wa mafao.

Alisema wameanza kufanya tathmini na mapitio ili kuhakikisha wastaafu wanalipwa kwa wakati.

"Mifumo mbalimbali imeanzishwa, hivi karibuni tutaanza ziara ya mkoa kwa mkoa kusikiliza kero za wastaafu na kuhakiki taarifa mbalimbali ili wapate mafao yao kwa wakati," alisema.

Katambi aliongeza kuwa ni wajibu wa mifuko kutunza kumbukumbu sahihi za wanachama wake na kuwasihi waajiri kuwasilisha michango kwa wakati ili kupunguza usumbufu kwa watumishi wanapostaafu.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itamaliza kero ya kuchelewesha mafao kwa wastaafu.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali za kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ikiwa ni pamoja na kutoa hati fungani ya Sh. trilioni 2.17 ambazo zitaimarisha mtiririko wa mapato na kuwezesha kutoa mafao kwa wakati.

Vilevile, Katambi alisema kuanzia Julai Mosi, 2021 hadi Aprili 30, 2022, wastaafu na wanufaika 24,757 wa NSSF wamelipwa Sh. bilioni 78 na wanufaika 42,427 wa PSSSF wamelipwa Sh. trilioni 1.99.

Alisema serikali inawahakikishia wastaafu wote nchini kuwa itaendelea kuwalipa mafao yao.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mpanda Vijijini (CCM), Moshi Kakoso, alisema wafanyakazi wa TAZARA wamekuwa wakiidai serikali mafao yao na wamechangia michango yote lakini TAZARA ilikuwa haipeleki na kuhoji serikali inawasaidiaje wafanyakazi hao ambao wengi wao wamefariki dunia.

Naibu Waziri Katambi, akijibu swali hilo, alisema serikali itaendelea kushughulikia suala hilo.



Mbunge wa Jimbo la Mvumi, Livingstone Lusinde, akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yaonyesha njia Vwawa kuwa manispaa

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ameshauri Mkoa wa Songwe kufuata taratibu za kuwasilisha maombi yao ya kupandisha Mji wa Vwawa kuwa manispaa.

Silinde alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga.

Katika swali lake, Hasunga alisema Mkoa wa Songwe kwa muda mrefu hauna manispaa na kuhoji ni lini Halmashauri ya Mji wa Vwawa itapandishwa kuwa manispaa.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema maombi hayo yawasilishwe kwa mamlaka husika ambayo kwa sasa imejikita kuboresha maeneo mengine.

"Tufuate taratibu na tutashauri mamlaka namna bora ya kulitekeleza zaidi," Silinde alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Constantine Kanyasu, alihoji ni lini Mji wa Geita utakuwa manispaa kwa kuwa taratibu zote zimekamilika na umefikia viwango vya kupewa hadhi ya manispaa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Silinde, alisema TAMISEMI ilipokea mapendekezo ya kupandisha hadhi Halmashauri ya Mji Geita kuwa manispaa.

"Mapendekezo hayo yalifanyiwa uhakiki na timu ya wataalamu kutoka OR-TAMISEMI. Kati ya vigezo 21, Halmashauri ya Mji wa Geita ilikuwa imekidhi vigezo 18, sawa na asilimia 85," alisema.

Silinde alitaja vigezo ambavyo havikuwa vimefikiwa na Mji wa Geita kuwa ni pamoja na kutokuwa na Mpango Kabambe wa Uendelezaji Mji, eneo lililopimwa lisipungue asilimia 75 ya eneo lote kutofikia asilimia 75 zinazohitajika za wakazi waliokuwa wameunganishwa na huduma ya maji.

"Hivyo, halmashauri hii haikuweza kupandishwa hadhi kwa kuwa ililazimu kukidhi vigezo vyote kwa pamoja kwa mujibu wa mwongozo wa kuanzisha maeneo ya utawala wa mwaka 2014 ili kupandishwa hadhi ya kuwa halmashauri ya manispaa," Silinde alibainisha.




Habari zote na Augusta Njoji

# Mbunge aona shida jela ukaguzi wa kuvua nguo

MBUNGE wa Viti Maalum, Nusrat Hanje, ameitaka serikali kujenga chumba maalum cha ukaguzi kwenye magereza badala ya wafungwa na mahabusu kuvua nguo hadharani.

Vilevile, amesema uchakavu wa nguo za wafungwa unawalazimu baadhi ya wanawake kurithi nguo za ndani za wenzao waliomaliza kifungo.

Akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jijini hapa jana, mbunge huyo alisema wafungwa na mahabusu wamekuwa wakifanyiwa ukaguzi hadharani kwa kuvua nguo zote bila kujali umri wao.

Mbunge huyo alisema kwa uzoefu wake, kuna uwezekano wa kuwakagua kwa kuwatenganisha au kuweka chumba maalum lakini serikali haifanyi hivyo.

"Ni kwanini serikali isitenge chumba maalum cha kuwakagua na kuwatenganisha ili kujenga staha na haki za binadamu?" mbunge huyo alihoji.

Pia alihoji mkakati wa serikali kuhakikisha inapeleka mavazi ya wafungwa pamoja na magodoro na mablanketi ili kuwaondolea adha inayowakabili.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alisema katika ukarabati na ujenzi wa magereza utakaofanyika, utazingatia umuhimu wa kuwatenganisha wafungwa wanawake na wanaume wakati ukaguzi unapofanyika.

Kuhusu mavazi, alisema kwa mwaka 2022/23, bajeti imeongezwa na kwenye maeneo ambayo yalikuwa hayapati fedha ikiwamo eneo la mavazi ya wafungwa, yamepewa kipaumbele.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum, Agnesta Kaiza, alihoji mpango wa serikali kukarabati magereza ili kulinda haki za wafungwa na waliopo mahabusu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Sagini alisema serikali kupitia Jeshi la Magereza imejipanga kukarabati magereza kwa kutumia fedha za vyanzo vya ndani na fedha inayotengwa kwenye bajeti kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Alisema katika mwaka 2021/22, serikali ilitenga Sh. milioni 840 kwa ajili ya ukarabati wa magereza matano ambayo ni Maweni, Isanga, Kondoa, Lindi na Mkuza na imetumia vyanzo vya ndani kukarabati magereza ya Rombo, Ukonga, Mkono wa Mara, Kwitanga, Idete, Mbigili, Shinyanga, King'ang'a, Butimba, Luanda, Liwale na Babati.

Alisema kuwa mwaka wa fedha 2022/23, Jeshi la Magereza limetenga Sh. bilioni 4.569 kujenga magereza sita ya wilaya za Kilosa, Kaliua, Karatu, Kakonko, Gairo na Msalato.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti maalum (CCM), Tekla Ungele, alihoji mpango wa serikali kuboresha miundombinu ya Gereza la Liwale kwa kuwa limejengwa kwa kutumia miti.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema serikali kupitia Jeshi la Magereza imeanza kuboresha miundombinu ya gereza hilo kwa kutumia fedha za vyanzo vya ndani.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Aprili 12, mwaka huu, inabainisha kuwapo msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu katika magereza mbalimbali nchini, pia hali mbaya ya miundombinu ya Jeshi la Magereza.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI



**MHE. PROF. MAKAME MBARAWA (MB)**
WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI



**MHE. GODFREY KASEKENYA (MB)**
NAIBU WAZIRI (UJENZI)



**MHE. ATUPELE MWAKIBETE (MB)**
NAIBU WAZIRI (UCHUKUZI)



**BALOZI MHA. AISHA AMOUR**
KATIBU MKUU (UJENZI)



**BW. LUDOVICK NDUHIYE**
NAIBU KATIBU MKUU (UJENZI)



**BW. GABRIEL MIGIRE**
KATIBU MKUU (UCHUKUZI)



**DKT. ALLY POSSI.**
NAIBU KATIBU MKUU (UCHUKUZI)

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. ***Mheshimiwa Spika***, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupa kibali cha kukutana leo tukiwa wazima wa afya njema ili kujadili hoja ya bajeti ya Wizara ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi uliotukuka ambao ameuonesha tangu alipochukua kijiti cha kuongoza Taifa hili tarehe 19 Machi, 2021. Uongozi wa Rais wa Awamu ya Sita umedhihirika kuwa wenye umakini wa hali ya juu, wenye maono, ujasiri, maarifa na mikakati ya kuleta mabadiliko chanya na ya haraka katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Mwenyezi Mungu amjalie Rais wetu afya njema ili aweze kutekeleza majukumu yake.

4. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kumpongeza Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango kwa jinsi anavyoendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuimarisha umoja wa kitaifa. Nimtakie kila la heri katika kutekeleza majukumu yake.

5. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kumpongeza wa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, kwa uongozi wake mahiri na makini. Sote ni mashuhuda wa kazi nzuri anayoifanya katika utekelezaji wa majukumu yake ndani na nje ya Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima kubwa nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyokuwa nayo juu yangu kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Naomba kumhakikishia kuwa mimi pamoja na wenzangu tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba tunaendeleza Sekta za Ujenzi na Uchukuzi ili kuweka mazingira wezeshi kwa sekta nyingine za kiuchumi kijamii kuchangia katika maendeleo ya Taifa na kufikia malengo tuliyojiwekea kupitia miongozo mbalimbali ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020.

7. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kuwa Naibu Spika. Hakika mnatosha na tuna imani kubwa kwamba chini ya uongozi wenu Bunge hili litatekeleza majukumu yake kwa umahiri na weledi mkubwa. Aidha, niwapongeze Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa namna wanavyolisimamia na kuliongoza Bunge letu Tukufu ili litimize majukumu yake ya kushauri na kuisimamia Serikali.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Kamati hii imekuwa msaada mkubwa sana kwa kutoa maoni na ushauri katika kuboresha utendaji wa Wizara. Aidha, uchambuzi wa Kamati kwenye Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umetusaidia kwa kiasi kikubwa kuandaa Bajeti ya Wizara kwa ubora wa hali ya juu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha aliyeteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya salamu hizo nichukue fursa hii kutoa mkono wa pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu Marehemu Elias John Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Marehemu aliwahi kuhudumu katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kama Naibu Waziri kuanzia mwaka 2016 hadi alipoteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tarehe 05 Desemba, 2020. Sisi katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika kuendeleza miundombinu ya barabara. Aidha, ninatoa mkono wa pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Mbunge mwenzetu Marehemu William Ole Nasha ambaye alikuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro. Pia, natoa pole kwa kifo cha Marehemu Irene Alex Ndyamukama, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mkoa wa Rukwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya uendelea na hotuba yangu, nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya Sekta za Kijamii na Kiuchumi kwa mwaka 2021/2022 na mwelekeo kwa mwaka 2022/2023. Aidha, nawapongeza Mawaziri wote waliotangulia kwa mawasilisho mazuri ya hotuba za Wizara wanazozisimamia.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### B-1 SEKTA YA UJENZI (FUNGU – 98)

**Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka 2021/2022**

***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/22, Sekta ya Ujenzi ilitengewa jumla ya Shilingi **38,540,787,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi 31,578,893,459.84,** sawa na asilimia **81.94** zilikuwa zimetolewa na Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeleo, Sekta ya Ujenzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 1,588,703,487,200.00**. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi 1,288,703,487,200.00** fedha za ndani na **Shilingi 300,000,000,000.00** fedha za nje. Hadi Aprili, 2022 fedha za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 1,532,703,487,200.00** sawa na asilimia **96.48**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,232,741,391,541.94** ni fedha za ndani na **Shilingi 299,962,095,658.06** ni fedha za nje.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kutekeleza miradi ya barabara kuu inayohusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa **kilometa 467.11** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **14** pamoja na ukarabati wa **kilometa 32.47** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Hadi kufikia

Aprili, 2022 ujenzi wa **kilometa 216.26** za barabara kuu kwa kiwango cha lami ulikuwa umekamilika, sawa na asilimia **46** na ukarabati wa **kilometa 2.5** sawa na asilimia **8** za Barabara Kuu. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja makubwa manne (**04**) umekamilika na madaraja mengine yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara za mikoa, Wizara kupitia TANROADS ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami jumla ya **kilometa 103.0** ambapo **kilometa 72.2** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 30.8** zilipangwa kujengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi nyingine ni ukarabati kwa kiwango cha changarawe jumla ya **kilometa 1,124.3**. Kati ya hizo, **kilometa 698.3** pamoja na madaraja/makalavati **34** yalipangwa kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 426** pamoja na madaraja/makalavati **32** yalipangwa kujengwa au kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Hadi Aprili, 2022 jumla ya kilometa **34.8** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa **307.41** zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Utekelezaji wa miradi ya madaraja upo katika hatua mbalimbali. Aidha, Mtandao wa barabara nchini una kilometa 36,361.95 ambapo kati ya hizo, kilometa 11,512.90 ni za lami na kilometa 24,849.05 ni za changarawe. Pia, miradi inayoendelea ina jumla ya kilometa 1206.525 na kati ya hizo kilometa 221.05 ujenzi wake umekamilika kwa kiwango cha lami/zege.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara vilevile ilipanga kufanya matengenezo ya kawaida kwa **kilometa 33,171.89,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 4,783.72,** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 549.38** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,291** katika barabara kuu na barabara za mikoa. Kazi nyingine ni shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na eneo la hifadhi za barabara na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu. Hadi Aprili, 2022 mpango wa matengenezo katika barabara kuu na za mikoa ulikuwa umekamilika kwa asilimia **30.** Vilevile, Wizara inaendelea na utoaji wa vibali vya usafirishaji barabarani wa mizigo maalum nchini kwa kutumia mfumo ujulikanao kama *Special Load Permit System.* Hadi Aprili, 2022 jumla ya vibali **35,818** vilitolewa na jumla ya **Shilingi bilioni 12.80** zilikusanywa kutokana na tozo ya upitishaji wa mizigo maalum.

16. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa Ujenzi wa Madaraja Makubwa ambapo hadi Aprili, 2022, miradi iliyokamilika ni ujenzi wa Daraja la Tanzanite (Dar es Salaam), Daraja la Sibiti (Singida), Daraja la Kiyegeya (Morogoro), Daraja la Magufuli (Morogoro), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Momba (Rukwa), Daraja la Mlalakuwa (Dar es Salaam), Daraja la Magara (Manyara), Daraja la Lukuledi (Lindi) na Daraja la Mara. Miradi mingine iliyokamilika ni Usanifu wa kina wa daraja la Simiyu (Mwanza), Daraja la Mitomoni (Ruvuma), Daraja la Godegode (Dodoma), Daraja la Sukuma (Mwanza), Daraja la Mkenda (Ruvuma), Daraja la Sanza (Singida) na Daraja la Mtera (Dodoma).

Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa Daraja la Msingi (Singida) ambalo utekelezaji wake umefikia asilimia 81 na ununuzi wa Madaraja ya Chuma uko katika hatua za mwisho. Aidha, kazi ya usanifu wa kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) inaendelea. Kuhusu ujenzi wa barabara unganishi katika Daraja la Sibiti (Singida), taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

*(Utekelezaji wa miradi ya Barabara na Madaraja umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 13 hadi wa 51**).*

**Vivuko na Majengo ya Serikali**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) iliendelea kutekeleza miradi ya ***ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko.*** Hadi Aprili, 2022, miradi iliyokamilika ni upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia upande wa Nyamisati na ujenzi wa miundombinu ya Kayenze – Bezi upande wa Kayenze.

Miradi inayoendelea ni ujenzi wa maegesho ya Kayenze (Kanyinya); maegesho ya Zumacheli katika kivuko cha Chato (Nkome) na ujenzi wa maegesho upande wa Mafia. Vilevile, ukarabati wa maegesho ya vivuko unaendelea katika vituo vya Magogoni (Kigamboni), Iramba (Majita) na Nyakarilo (Kome).

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***ununuzi wa vivuko,*** hadi Aprili, 2022, ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kisorya na Rugezi (Mwanza) ulikuwa katika hatua za awali. Vivuko vitakavyotoa huduma kati ya Ijinga – Kahangala (Magu), Bwiro – Bukondo (Mwanza), Nyakarilo – Kome (Geita), kivuko cha pili cha Nyamisati – Mafia (Pwani) na kivuko cha Magogoni vipo katika hatua mbalimbali za manunuzi.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***Ukarabati wa Vivuko*** iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22 hadi Aprili, 2022, ukarabati mkubwa wa MV Mafanikio na MV Sabasaba umekamilika. Miradi inayoendelea ni ukarabati wa MV Musoma, Old MV Ruvuvu, MV Nyerere na MV Kilombero II pamoja na ukarabati wa mitambo ya ICoT. Miradi iliyo katika hatua za manunuzi ni pamoja na ukarabati MV Mara, MV Ujenzi, MV Ruhuhu, MV Misungwi, MV Kome II, MV Kyanyabasa na MV Tanga.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2021/22. Hadi Aprili, 2022, ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Jijini Dodoma ulifikia asilimia 90 na ujenzi wa nyumba 150 za makazi ya Watumishi wa Umma katika eneo la Nzuguni Jijini Dodoma ulifikia asilimia 90. Aidha, hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa nyumba za Majaji Kilimanjaro (asilimia 70), Mtwara (asilimia 75), Shinyanga (asilimia 75) na Tabora (asilimia 98.5).

21. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa nyumba 40 za Viongozi Dodoma umefikia asilimia 75.7. Kwa upande wa ukarabati wa nyumba 30 za Viongozi mikoani pamoja na matengenezo kinga ya majengo ya Magomeni Kota, utekelezaji umefikia asilimia 98. Ukarabati wa nyumba 40 kati ya 66 zilizohamishiwa TBA kutoka CDA unaendelea ambapo hadi Aprili, 2022 ulifikia asilimia 70. Aidha, utekelezaji wa ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI/NHC katika mikoa 20 zilizohamishiwa TBA umefikia asilimia 32. Vilevile, ununuzi wa samani kwa nyumba za Ikulu Ndogo umefanyika katika Mkoa wa Dodoma.
*(Utekelezaji wa miradi ya Vivuko na Majengo ya Serikali umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 52 hadi wa 55; Aya ya 109 hadi ya Aya 115**).*

**Viwanja vya Ndege**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza kazi za ujenzi pamoja na uboreshaji wa viwanja vya ndege katika mikoa mbalimbali nchini. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Songea, Mtwara, Iringa, Musoma na Songwe. Vilevile, mkataba wa Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Mkoani Dodoma umesainiwa na Mkandarasi yupo katika hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi.

*(Utekelezaji wa miradi ya Viwanja vya Ndege umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 57 hadi wa 61; Aya ya 119 hadi Aya ya 127**).*

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Bodi ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 908,355,896,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 635,849,127,200** ni kwa ajili ya kugharamia kazi za matengenezo na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Aidha, kiasi cha **Shilingi 272,506,768,800** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) ilitengewa **Shilingi 63,038,082,471**; TANROADS **Shilingi 567,342,742,235**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 27,016,321,059** na

TARURA **Shilingi 243,146,889,529**. Mgawanyo huo ni baada ya kutoa **Shilingi 7,811,860,706.00** kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa Mfuko kwa mujibu wa sheria.

***24. Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2022, Bodi imekusanya jumla ya **Shilingi 541,641,298,899.00** sawa na **asilimia 85** ya bajeti ya mwaka. Makusanyo hayo ya Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 yaliongezeka kwa **asilimia 6** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2020/21. Ongezeko hili limechangiwa zaidi na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kutokana utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati pamoja na kupungua kwa maambukizi ya virusi vya UVIKO 19.

*(Utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 61 hadi wa 80; Aya ya 128hadi Aya ya 168**).*

**B-2 SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU – 62)**

***25. Mheshimiwa*** Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 91,743,411,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi 71,098,606,554.68** sawa na **asilimia 77.5**. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,028,306,410,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,828,306,410,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 200,000,000,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2022 jumla ya **Shilingi 2,515,524,352,520.58** sawa na **asilimia 124** zilikuwa zimetolewa.

*(Tofauti ya matumizi ya fedha za ndani za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa ni kutokana na **uwepo wa hati za madai ya Wakandarasi wa ujenzi wa reli ya SGR** pamoja na kuanza ujenzi wa reli ya SGR kwa vipande viwili vya **Makutupora - Tabora** (**Km 368**) na **Mwanza – Isaka** (**Km 341**))* katika mwaka wa fedha 2021/2022).

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA UTOAJI HUDUMA**

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya barabara**

***26. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kutekeleza mpango wa kuwasajili madereva na wahudumu wa magari ya biashara kwa lengo la kuwarasimisha ili kuboresha ufanisi katika sekta ya usafirishaji. Hadi kufikia Aprili, 2022 jumla ya madereva wa magari ya biashara 9,933 walikuwa wamesajiliwa. Vilevile, Serikali kupitia LATRA na eGA inaendelea kutengeneza Mfumo utakaotumika kuthibitisha madereva wanaoendesha vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara.

***27. Mheshimiwa Spika,*** LATRA imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi ya masafa marefu na treni kwa kutumia mfumo maalum (Vehicle Tracking System - VTS). Hadi mwezi Aprili, 2022, jumla ya mabasi 6,956 na vichwa vya treni 18 vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo huo. Aidha, kazi ya kuboresha mfumo na kuufunga kwenye mabasi yanayotoa huduma kwenye njia fupi inaendelea. Miongoni mwa faida za mfumo huu ni kuimarisha usalama barabarani na kwenye reli; Kuboresha ubora wa huduma kwa wateja; Kusaidia wasafirishaji kusimamia biashara ya uchukuzi kikamilifu; na Kudhibiti matumizi ya mafuta kwenye vyombo husika na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji (kutokana na kudhibiti mwendokasi wa magari, gari linalotumia VTS linapunguza matumizi ya mafuta kati ya asilimia 20 hadi 30 kutokana na kuendeshwa kwa mwendo wa wastani).

*(Utendaji katika udhibiti wa usafiri kwa njia ya barabara katika mwaka 2021/22 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 83 hadi wa 88 Aya ya 173 hadi 179**).*

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

***28. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeendelea kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za usafiri wa reli kwa ajili ya kutoa huduma nchini na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na DRC. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili 2022, TRC ilisafirisha tani 337,617 za mizigo ikilinganishwa na tani 257,747 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 30.1. Sababu za ongezeko la mzigo ni uboreshaji wa miundombinu ya reli na mabehewa 240 ya mizigo.

***29. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili 2022, idadi ya abiria wa treni waliohudumiwa katika Jiji la Dar es Salaam kati ya Stesheni ya Kamata - Ubungo - Pugu ni 2,570,740 ikilinganishwa na abiria 2,307,394 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 11.4. Ongezeko hilo limetokana na uboreshaji wa huduma.

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2021/2022, tuliahidi kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (km 1,219), hususan katika vipande viwili vya awali, Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) na Morogoro hadi Makutupora (Km 422). Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa vipande hivyo vya reli na hadi kufikia Aprili, 2022 kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro kimefikia asilimia 96.54 na tayari majaribio ya kuingiza umeme wa kuendeshea treni kwenye mfumo yamekwishaanza. Aidha, kwa kipande cha reli kutoka Morogoro hadi Makutupora (Km 422), kazi ya ujenzi imefikia asilimia 85.02 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2023.

***31. Mheshimiwa Spika***, kuhusu kipande cha Makutupora hadi Tabora chenye urefu wa km 368 (Km 294 njia kuu na km 74 njia za kupishania), Mkataba wa Ujenzi wa kipande hicho ulisainiwa tarehe 28 Disemba, 2021 kati ya TRC na Mkandarasi na maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea. Kwa upande wa ujenzi wa kipande kilichobaki katika awamu ya kwanza cha Tabora – Isaka (Km 165), Serikali ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa Mkandarasi.

***32. Mheshimiwa Spika***, kuhusu kipande cha reli cha Mwanza - Isaka (Lot. 5) chenye urefu wa kilomita 341 (kilomita 249 za njia kuu na kilomita 92 njia za kupishania treni) ujenzi umefikia asilimia 6.8.

***33. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi wa awamu ya pili ya reli ya *Standard Gauge* ambapo ujenzi wa kipande cha Tabora – Kigoma (Km 411) upo katika hatua za manunuzi ya Mkandarasi. Aidha, Serikali ya Tanzania na Burundi zimesaini makubaliano ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa njia ya reli ya Uvinza-Musongati-Gitega (Km 282). Vilevile, Serikali ya Burundi na DRC tayari zilishatangaza zabuni ya kufanya upembuzi yakinifu kutoka Gitega hadi Kindu-DRC ili reli hiyo iweze kutoka Bandari ya Dar es Salaam mpaka Kindu-DRC.

*(Utekelezaji wa miradi ya reli ya Kati kupitia TRC umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 89 hadi wa 95 Aya ya 180 hadi 189** ).*

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

***34. Mheshimiwa Spika,*** huduma za kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (Tanzania Zambia Railway Authority - TAZARA).

***35. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 180,597 za mizigo ikilinganishwa na tani 173,490 zilizosafirishwa kwa kipindi kama hicho 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 4.0. Ongezeko hili limechangiwa na kukarabatiwa kwa injini saba (7) zilizofungwa vipuri vipya (42 Traction Motors) pamoja na matengenezo ya njia ya reli hasa kwenye maeneo korofi ya reli.

*(Utekelezaji wa miradi ya reli ya TAZARA umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 95 hadi wa 98 Aya ya 190 hadi 193** )*

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya Maji**

***36. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kudhibiti ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira majini utokanao na shughuli za usafiri majini,

pamoja na kulinda maslahi mapana ya nchi kuhusu Sekta ya usafiri majini.

37. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) imehudumia meli 388 ikiwa ni zaidi ya lengo lililopangwa la kuhudumia meli 340. Hii, ni sawa na meli 48 zaidi ya lengo lililopangwa, sawa na asilimia 14%. Aidha, Shirika limefanikiwa kuhudumia mabaharia 956 wanaotoka melini kwa sababu mbalimbali ikiwemo mapumziko ya likizo, kuisha kwa muda wa mikataba ya kazi na pia mabaharia wanaoingia nchini kwa ajili ya kuja kuanza rasmi kazi melini

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TASAC imeimarisha uratibu wa zoezi la utafutaji na uokoaji katika ajali zinazotokea majini kwa kutoa elimu kuhusu umuhimu na majukumu ya Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini (Maritime Rescue Coordination Centre – MRCC/ISC) kilichopo Dar es Salaam pamoja na kushiriki mikutano ya Kitaifa na Kikanda kwa lengo la kuweka mikakati ya kufanikisha zoezi la utafutaji na uokoaji endapo ajali inatokea baharini. Aidha, Shirika limeanza kufanya upembuzi yakinifu kwa mwaka huu wa fedha 2021/22 kwa ajili ya ujenzi wa boti tatu (3) za Utafutaji na Uokoaji (SAR) zitakazotumika kwenye Maziwa Makuu (Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa). Baada ya upembuzi yakinifu na ununuzi wa boti hizo kukamilika, mgawanyo wa boti hizo utafanyika katika maziwa husika. katika Bahari ya Hindi na ununuzi wa boti mbili (2) kwa ajili ya kutumika katika Ziwa Victoria.

*(Utendaji katika udhibiti wa usafiri kwa njia ya maji kwa mwaka 2020/2021 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba* ***Ukurasa wa 98 hadi 104 Aya ya 194 hadi 204*** *)*

**Huduma za Uchukuzi katika Maziwa**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri kwenye Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili 2022, Kampuni hiyo ilisafirisha abiria 242,107 ikilinganishwa na abiria 230,149 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Aidha, jumla ya tani za mizigo 20,484.67 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani za mizigo 15,965.32 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 28.31. Ongezeko hilo limetokana na Kampuni kujitangaza.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya MSCL imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa meli ya MV Mwanza (Hapa Kazi Tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria, ambao ujenzi wake umefikia asilimia 66; Mradi wa ukarabati mkubwa wa meli ya MV Umoja yenye uwezo wa kubeba tani 1,200 za mizigo ambayo hufanya safari zake kati ya Tanzania na nchi jirani za Kenya na Uganda katika Ziwa Victoria, utekelezaji wake umefikia asilimia 25; na Mradi wa ukarabati mkubwa wa meli ya MT Sangara katika Ziwa Tanganyika yenye uwezo wa kubeba mafuta lita 400,000 inayofanya safari zake kati ya Tanzania na nchi jirani za DR Congo, Burundi na Zambia, utekelezaji wake umefikia asilimia 19.4.

*(Utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba* ***Ukurasa wa 105 hadi wa 107 Aya ya 207 hadi 209*** *)*

**Huduma za Bandari**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kusimamia Bandari za Mwambao na za Maziwa Makuu kwa kuendeleza miundombinu na huduma za kibandari; kuweka viwango na masharti kwa watoa huduma za bandari nchini; kusimamia na kudhibiti huduma za bandari; kulinda mazingira na usalama wa bandari kwa viwango vinavyokubalika; pamoja na kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji kuwekeza katika sekta ya bandari. Aidha, Mamlaka imeendelea kutangaza bandari kimasoko pamoja na kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili 2022, TPA ilihudumia shehena ya tani za mapato milioni 11.341 na kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 888.93 ikilinganishwa na shehena ya tani za mapato (revenue) milioni 10.01 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la mapato la asilimia 18.32. Aidha, jumla ya magari 162,340 yalipakuliwa katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na magari 119,854 yaliyopakuliwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 35.5.

*(Utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa bandari zilizo kwenye mwambao wa bahari ya Hindi na Maziwa Makuu umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba* ***Ukurasa wa 107 hadi wa 112 Aya ya 210 hadi 218****)*

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usafiri wa Anga (Tanzania Civil Aviation Authority - TCAA) imeendelea kudhibiti huduma za usafiri wa anga ikiwa ni pamoja na Viwanja vyote vya Ndege nchini. Lengo ni kuimarisha utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege. Aidha, TCAA imeendelea kusimamia masuala ya kiusalama na kiuchumi katika utoaji wa huduma za usafiri kwa njia ya anga na uongozaji ndege kupitia vituo 14 vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga, Songea na Kilimanjaro.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili 2022, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga ni 1,748,278 ikilinganishwa na abiria 2,964,636 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na upungufu wa asilimia 41. Sababu kubwa ya kupungua wa abiria ni uwepo wa janga la UVIKO - 19.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege 58 vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha, TAA imeendelea kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa viwango; kuboresha huduma za ulinzi na usalama katika viwanja hivyo pamoja na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi. Kwa upande wa Kiwanja cha Kimaifa cha Kilimanjaro (KIA), jukumu la kuendesha na kuendeleza Kiwanja hicho limeendelea kusimamiwa kwa Kampuni ya Kuendeleza Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (KADCO).

**Huduma za Usafiri kwa njia ya Anga**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imeendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya Tanzania. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, Serikali ilikamilisha ununuzi wa ndege tatu (3) mpya na kuzikabidhi ATCL. Ndege hizo ni Dash 8 Q400 ndege moja (01) yenye uwezo wa kubeba abiria 76 na ndege mbili (2) aina ya Airbus A220-300 zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja. Kuongezeka kwa ndege hizo kumeifanya ATCL kuwa na jumla ya ndege mpya 11 kufikia Aprili, 2022 ikilinganishwa na ndege 8 zilizokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2020/21.

47.

***(****Maelezo kuhusu utendaji katika usafiri na uchukuzi kwa njia ya anga kwa mwaka 2020/2021 yametolewa katika Kitabu cha Hotuba* ***Ukurasa wa 113 hadi 131 Aya ya 219 hadi 249)***

**Huduma za Hali ya Hewa**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imeendelea kusimamia, kudhibiti na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa hapa nchini. Kwa sasa usahihi wa utabiri wa hali ya hewa umefikia asilimia 88.3 ambao ni juu ya asilimia 70 ya kiwango cha usahihi kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani. Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa kuwa na mtandao wa Rada saba (7) za hali ya hewa hapa nchini kama ilivyoelezwa kwenye Ilani ya CCM mwaka 2020. Malipo ya ununuzi wa Rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa Kilimanjaro na Dodoma yamefanyika kwa asilimia 80. Utengenezaji wa rada za hali ya hewa zinazotarajiwa kufungwa Kigoma na

Mbeya upo katika hatua za mwisho nchini Marekani. Malipo yamefanyika kwa asilimia 80 kwa ajili ya uboreshaji wa mifumo ya rada za Dar es Salaam na Mwanza ili kuendana na teknolojia ya kisasa.

*(Utekelezaji wa miradi na huduma za hali ya hewa umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba **Ukurasa wa 132 hadi 135 Aya ya 250 hadi 253**)*

**TAASISI ZA MAFUNZO**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi za mafunzo zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi na uchukuzi zimeendelea kutoa mafunzo katika kujenga uwezo wa wataalam kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu na utoaji wa huduma. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Mafunzo zinazosimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 umeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba kuanzia ***Ukurasa wa 135 hadi 143*** **Aya ya 254 hadi 269**

**C. CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO**

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kukabiliana nayo imeoneshwa katika Kitabu cha Hotuba ***Ukurasa wa 148 hadi wa 156*** **Aya ya 275**

**D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2022/2023 kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

**D.1.1 SEKTA YA UJENZI**

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) imetengewa **Shilingi 44,293,050,000.00** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Bajeti ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi imetengewa **Shilingi 1,421,542,185,800.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,168,576,368,800.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 252,965,817,000.00** ni za fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizotengwa, **Shilingi 599,756,467,800.00** ni fedha kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 568,819,901,000.00**.

*(Mgawanyo wa fedha za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyoonyeshwa katika **Viambatisho Na.1 na Na. 2 vya Hotuba**)*

*(Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi umeonyeshwa katika **Viambatisho Na. 3 na 4.** Aidha, mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D**).*

**D.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI**

**Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 2,400,781,440,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 94,546,502,000.00** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,306,234,938,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 6.**

**E. SHUKRANI**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22, Wizara imepata ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali wakati ikitekeleza malengo yake. Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wote walioshirikiana nasi kimawazo na kwa vitendo. Shukrani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imesaidia katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, wananchi na wadau mbalimbali waendelee na moyo huo katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ili tuweze kuendeleza shughuli za Wizara hii ambazo ni muhimu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa ***Mhandisi Godfrey*** **Msongwe Kasekenya (Mb.)** na Mheshimiwa **Atupele Fred Mwakibete (Mb.);** Makatibu Wakuu Bwana **Gabriel Joseph Migire** (Uchukuzi) na Balozi Mhandisi **Aisha Salim Amour** (Ujenzi); Naibu Makatibu Wakuu Bwana **Ludovick James Nduhiye** (Ujenzi) na Dkt. **Ally Possi** (Uchukuzi). Vilevile, kipekee napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara. Naomba waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kufikia malengo ya Wizara na ya Taifa kwa ujumla.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Washirika mbalimbali wa Maendeleo wamekuwa wakichangia katika utekelezaji wa Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwatambua Washirika mbalimbali wa Maendeleo ambao wamechangia katika utekelezaji wa Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuwatambua wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Umoja wa Nchi za Ulaya, "Third World Organization for Women in Science (TWOWS)", UNESCO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (FCDO), Uholanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF, PSSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali; Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

**57** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Mhe. Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.mwt.go.tz**).

**F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa bajeti yake kama ifuatavyo:

**F.1. SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) inaombewa **Shilingi 1,465,835,235,800.00.** Kati ya hizo, **Shilingi 44,293,050,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na **Shilingi 1,421,542,185,800.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**F.2. SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) inaombewa jumla ya **Shilingi 2,400,781,440,000.00**. Kati ya hizo, **Shilingi 94,546,502,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,306,234,938,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 **(Kiambatisho Na. 1-6)** ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza Miradi hiyo. Naomba kitabu kizima cha Hotuba yangu ya bajeti pamoja na viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya hoja hii.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, Naomba kutoa hoja.





# Waziri apigia chapuo mkataba biashara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara, Maendeleo na Viwanda, Omar Said Shaaban, amesema utekelezaji wa mkataba wa soko la eneo huru la kibiashara Afrika (AFCFTA), utasaidia kukuza fursa za kibiashara na kufikia malengo ya kuwa na soko la pamoja.

Amesema baada ya kuridhia mkataba huo, serikali inaendelea kujipanga kwa utekelezaji ili kunufaika ipasavyo na fursa hizo na kwamba kwa sasa serikali inafanya uchambuzi wa kina kuhusu mkataba wa AFCFTA kwenye uchumi na kuandaa mkakati wa kitaifa.

Waziri Shaaban aliyasema hayo jana wakati akifungua warsha kwa wabunge, wawakilishi na viongozi wa serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar kuhusiana na mkataba wa eneo huru la biashara Afrika, uliofadhiliwa na Taasisi ya GIZ na Benki ya AFREXIM, iliyofanyika katika Hotel ya Sea Cliff, Unguja.

Alisema mkakati huo unakuwa shirikishi na jumuishi kwa masuala ya uchumi wa bluu, utalii na uzalishaji wa karafuu na viungo yanajitokeza vizuri kwenye mkakati huo ili sekta hizo zinufaike na soko la AFCFTA.

Lengo la warsha hiyo, alisema ni kutoa uelewa kwa watendaji hao ili kuona wanatambua fursa zilizopo zikiwamo za biashara na uwekezaji. Pia alisema lengo lingine ni kujenga uwezo wadau nchini kuhusu mkataba huo pamoja na fursa zake.

Alisema Tanzania kisheria ni wajumbe halali wa mkataba huo na umechangia kwa kiasi kikubwa kuamini kuwa itasaidia kuimarisha masuala ya kiuchumi kwa ajili ya nchi.

Waziri Shaban alisema serikali imefanya utafiti wa kina kuhusu mkataba huo unaohusisha zaidi ya nchi 50 ili kuwa shirikishi. Alisema miongoni mwao ni mpango wa nchi ndogo za visiwa hasa katika kufanikiwa kuzalisha na kuingiza sokoni bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwamo viungo.

Pia alisema kwa sasa serikali inajikita zaidi kuhakikisha inaendelea kutoa elimu kuhusiana na mkataba huo kwa wadau wa masuala mbalimbali ili kutambulika na kutoa matunda kama ilivyotarajiwa, ikiwamo namna ya kuzalisha na kutengeneza vifungashio vyenye ubora unaokubalikaa.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara wa Tanzania, Naibu Waziri Exaud Kihage, alisema wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itahakikisha inaelimisha jamii kuhusiana na mkataba huo ili kuleta manufaa kwa nchi.

Pia aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuridhia kufanyika warsha hiyo, ikiwa ni mwendelezo wa maono ya waasisi wa nchi akiwamo Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Naye Mwakilishi wa Benki ya AFREXIM, Dk. Emeka Ozomba, alisema kuwapo mifumo bora ya kibiashara na uchumi kutasaidia wananchi wa Afrika wapatao bilioni 1.3 kupata ajira kupitia biashara ya soko hilo.

Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya AfCFTA, Wamkele Mene, alisema lengo lao ni kutafuta njia bora ya kuimarisha masuala ya kibiashara katika Umoja wa Afrika sambamba na kufanya kazi kwa ushirikiano.

Baadhi ya washiriki wa warsha hiyo, walishauri umuhimu wa wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora kutokana na ushindani mkubwa wa bidhaa zitakazouzwa kupitia soko la dunia.

Mkataba wa AfCFTA ulitiwa saini katika Mkutano wa 10 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) uliofanyika MACHI 21, 2018 Kigali, Rwanda.

## Aliyedaiwa kumnajisi mwanawe akamatwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Liwale kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Zanzibar, limefanikiwa kumkamata mtuhumiwa anayedaiwa kumbaka mwanawe wa kumzaa (jina linahifadhiwa) mwenye umri wa miaka 11 na kukimbia.

Mtuhumiwa huyo, Kheri Mkombe (39), alidaiwa kufanya ukatili huo wiki moja iliyopita Fukoni Pangawe, mkoa wa Mjini Magharibi na kukimbilia mkoani Lindi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Abdallah Hussein Mussa, alisema jitihada za kumkamata mtuhumiwa huyo zinatokana na kitengo chake cha makosa ya kimtandao (cybercrime) pamoja na ushirikiano na wananchi.

Kamanda Abdallah alisema mtuhumiwa huyo baada ya kufanya tukio hilo, alikimbilia kusikojulikana na kukamatwa Mei 20 majira ya saa 7:00 mchana katika kijiji cha Likongowele, Liwale mkoani Lindi.

Alisema Jeshi la Polisi litahakikisha linafuata taratibu za kisheria na litakapokamilisha upelelezi, mtuhumiwa huyo atafikishwa katika vyombo vya sheria.

Mtuhumiwa huyo alidaiwa kutenda tukio hilo la kumwingilia kinyume na maumbile mtoto wake wa kike Mei 10, mwaka huu, majira saa 4:00 usiku huko Fuoni Pangawe.

Kamanda aliwapongeza wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vimeshiriki katika kufanikisha ukamataji wa mtuhumiwa huyo sambamba na vyombo vya habari ambavyo vimetumia nguvu ya kihabari kupaza sauti na kusikika katika kukemea na kuchukizwa na tukio hilo pamoja na matukio mengine ambayo yanakwenda kinyume cha sheria za nchi.




Mkuu wa Kitengo cha wateja binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili (wa tatu kulia), akikabidhi sehemu ya vifaa vya Studio na Tehama kwa Kamishna wa Utawala na Fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mbaraka Semwanza, Ilala jijini Dar es Salaam jana, vitakavyotumiwa na jeshi hilo, kutoa taarifa mbalimbali kwa umma. Wengine (kutoka kulia) ni Meneja Mwandamizi wa Huduma Mbadala, Benki ya CRDB, Mangire Kibanda, Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi Benki ya CRDB, Farida Hamza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Zimamoto, Puyo Nzalayamisi na Kamanda wa Jeshi hilo, Mkoa wa Ilala, Mrakibu Elisa Mugisha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atoa sababu ya visiwa kukodishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali iliona kuna haja ya kukaribisha sekta binafsi kuviendeleza visiwa vidogo na kutoa ajira hatimaye kuchangia pato la taifa.

Amesema hatua hiyo ilichukuliwa baada ya kuona visiwa hivyo kwa muda mrefu havikutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, kulinganisha na uzoefu wa nchi zingine za visiwa kama Maldives, Singapore, Malaysia pamoja na Caribbean.

Soraga aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi, aliyetaka kujua ni utaratibu gani uliofanyika kabla ya kukodishwa kwa visiwa hivyo vidogo. Alisema serikali iliamua kuimarisha uwekezaji katika visiwa vidogo ili kuimarisha maendeleo na ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Kwa mujibu wa Soraga, katika kufikia hatua hiyo, serikali iliwashirikisha kikamilifu wananchi na kuwapa habari kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kufanya mikutano na wananchi walioko katika visiwa hivyo.

"Mheshimiwa Spika, utaratibu uliotumika kuvikodisha visiwa vidogo ni wa njia ya wazi, kwa maana ya kwamba ni njia ya kutangazwa katika vyombo mbalimbali vikiwamo vya ndani na nje ya nchi. Katika utaratibu huu, wazabuni hupaswa kuonyesha nia kwa kila mwenye nia ya kuwekeza na kutaja aina ya mradi anaotaka kuwekeza na kiasi cha mtaji anachotaka kuwekeza," alisema.

Pia alisema kabla ya visiwa hivyo kukodishwa, vilifanyiwa tathmini na kupatiwa madaraja mahususi kwa kuzingatia masafa kutoka kisiwa kikuu, miundombinu iliyokuwapo (maji na umeme), matumbawe na rasilimali zingine za bahari zinazozunguka kisiwa, uoto wa asili na kuwapo kwa ufukwe wa mchanga.

Alisema kutokana na Sheria ya Ardhi iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi namba 12 ya mwaka 1992 pamoja na marekebisho yake, visiwa hivyo kwa utii wa sheria hiyo vitakodishwa kwa kipindi cha miaka 30.

"Kwa kuwa kila mwekezaji atapewa mkataba wa ukodishwaji wa ardhi, kwa mujibu wa sheria, serikali imeweka vigezo na masharti ya kuzingatiwa kwenye kila mkataba husika na kwa mazingira yake," alisema.

Alisema tayari serikali ilikuwa imeshatoa maelekezo kwamba shughuli za wananchi walizokuwa wanafanya ziendelee katika visiwa hivyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHARITY MBUKWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S.2655/0012 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA MARANATHA SEKONDARI MWAKA 2014.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/198973/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUZMA SALUM HASHAM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.743 DKK aina ya IST. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

**Taarifa ya Jeshi la Polisi.**

**KAH/TR/RB/256/2022.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASIJALA NDOGO YA MWANZA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MAOMBI MADOGO YA MADAI NO. 105 YA 2021**
**(LILILOTOKANA NA SHAURI LA MSINGI MADAI NA. 1/2019**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA)**
**SABINA CHACHA................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**

- **KASSIM ALLY............MJIBU MAOMBI WA 1.**
- **DORA YONA LUBAHULA...MJIBU MAOMBI WA 2.**

**KWA: KASSIM ALLY**
**P.O. Box 2926, MWANZA – Popote Ulipo.**

**KUITWA SHAURINI**

Fahamu ya kwamba, shauri tajwa hapo juu ambalo wewe ni mjibu maombi wa 1. Shauri limepangwa kusikilizwa mbele ya Mahakama hii tarehe 14/06/2022 saa 3:00 asubuhi. Hivyo unatakiwa kuhudhuria Mahakamani wewe mwenyewe au mwakilishi wako siku hiyo bila kukosa.

Kutokuhudhuria kwako kutaifanya Mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 19 Mwezi Mei, 2022.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

## KUPOTEA KWA CHETI



**DORIN E NGOWI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0328-021** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **MAWENZI** mwaka 1993,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa DAR/STA/RB/164986/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI DODOMA, Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 73/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SAID LUGENDO MASIMBUSI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA ZALHATA MIRAJI MAKANGE**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 08 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imtolewa leo tarehe 24/05/2022.**

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE OF KIVUKONI/AT KINONDONI (EXTENDED JURISDICTION)**

**EXTENDED LAND APPEAL NO.20 OF 2021**

**GERVAS BENARD LYENGI.........APPELLANT**

**VERSUS**

**UPONERA VILLAGE COUNCIL........................1st RESPONDENT**
**JOSEPH TUMAINI MZAVA.............................2nd RESPONDENT**
**GABENUS OCTAVIAN FIMBO........................3rd RESPONDENT**
**CHARLES KIHIYO..........................................4th RESPONDENT**

**TO.**
**UPONERA VILLAGE COUNCIL....................1st RESPONDENT**
**JOSEPH TUMAINI MZAVA............................2nd RESPONDENT**
**GABENUS OCTAVIAN FIMBO.......................3rd RESPONDENT**
**CHARLES KIHIYO.......................................4th RESPONDENT**

**WHEREAS:** the above named appellant has instituted an appeal against you, you are summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on 01st june 2022 before Hon.M MPAZE SRM to answer the said appeal: and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defense
**TAKE NOTICE:**that,in default of your appearance on that day FOR THE HEARING, the appeal will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this court,this 23rd day of may 2022.

M.MPAZE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
(WITH EXTENDED JURISDICTION)

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mwanamke mjamzito na watoto wake wauawa

**LAGOS,** NIGERIA

POLISI nchini Nigeria wamesema wanawasaka watu wenye silaha walioua takriban watu 12, akiwemo mwanamke mjamzito na watoto wake wanne, katika jimbo la kusini mashariki la Anambra.

Wamelaumu ghasia zinazoongezeka katika eneo hilo kwa watu wanaotaka kujitenga la Biafra.

Kiongozi wa jamii aliiambia BBC, kwamba mwanamke huyo mjamzito na watoto wake walikuwa wakirejea nyumbani kwa pikipiki wakati watu wenye silaha walipowavizia katika eneo la Orumba.

Watu wengine kadhaa pia waliuawa kwa kupigwa risasi katika matukio tofauti Jumapili jioni.

Polisi walisema wanachunguza. Mauaji hayo ambayo yamezua hasira kwenye mitandao ya kijamii.

Tukio hilo limetokea siku moja baada ya mwili wa mbunge wa eneo hilo na msaidizi wake kugunduliwa wiki moja baada ya kutekwa nyara.

Ghasia zinazozidi kusambaa kusini-mashariki mwa Nigeria, zinalaumiwa kwa kundi lililopigwa marufuku la The Indigenous People of Biafra ambalo linafanya kampeni kwa ajili ya jimbo kujitenga.

Kundi hilo limekanusha kuhusika na baadhi ya mashambulizi hayo. Hata hivyo, vikosi vya usalama pia vinakabiliana na makundi mbalimbali yenye silaha.

Wanamgambo wa Boko Haram na kundi lenye uhusiano na IS wanafanya kazi katika eneo hilo. Ukosefu wa usalama ulioenea unaleta wasiwasi wa usalama kabla ya uchaguzi . **BBC**

## Rwanda yadai kushambuliwa na DR Congo

**KIGALI,** RWANDA

JESHI la Rwanda limesema watu kadhaa wamejeruhiwa katika mashambulio yaliyotokea kati yao na wanajeshi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Rwanda ilisema ilikuwa imeomba timu ya kikanda ya waangalizi wa kijeshi ili kufanya uchunguzi wa haraka.

Taharuki kati ya nchi hizo mbili imeongezeka tangu mwezi Machi, wakati waasi wa kundi la M23 waliposhambulia ngome za jeshi la Congo.

Rwanda inakanusha madai kwamba inaunga mkono waasi hao.

Kundi hilo liliteka eneo la mashariki mwa DR Congo mwaka 2012 na 2013, kabla ya wapiganaji wake kufukuzwa na vikosi vya Congo na Umoja wa Mataifa.

Familia nyingi zimeacha makazi yao katika jimbo la Kivu Kaskazini-DRC nchini DR Congo, kuelekea mji wa mpakani wa Uganda wa Bunagana.

Mkuu wa shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi nchini Uganda, Joel Boutroue, aliambia BBC kwamba maelfu ya wakimbizi waliwasili Uganda siku ya Jumatatu. **BBC**



Wanajeshi wa Ukraine wakiongoza mapambano ya kuutetea mji wa Mashariki wa Donbas juzi. **PICHA AFP**

# Ukraine kupokea vinu vya kufyatulia makombora

**WASHINGTON,** MAREKANI

NCHI kadhaa za Ulaya zimekubali kutoa silaha mpya kwa Ukraine, ikiwemo, helikopta za mashambulizi, vifaru na mifumo ya kufyatulia makombora

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ulinzi wa Marekani Lloyd Austin, kufuatia mkutano wa Kikundi cha Ushauri kuhusu Usaidizi kwa Ukraine.

"Ninaishukuru sana Denmark kwa kutangaza kwamba itaipatia Ukraine vifaa vya kufyatua makombora ili kusaidia kulinda pwani," alisema.

Makombora ya kupambana na meli ya Marekani yana umbali wa kilomita 124-220. Kulingana na marekebisho, yanaweza kuzinduliwa kutoka kwa meli, manowari, ndege, mitambo ya pwani. Kasi ya kukimbia ya kombora hufikia mita 240.

"Pia ninashukuru kwa msaada muhimu wa Jamhuri ya Czech, ambayo hivi karibuni imetoa helikopta za mashambulizi, vifaru na mifumo ya makombora," Waziri huyo aliongeza.

Alisema nchi kadhaa zimetangaza zitasaidia kwa mifumo muhimu ya mizinga na makombora.

Nchi hizo ni Italia, Ugiriki, Norway na Poland.

"Niipongeze Uingereza kwa uongozi na usaidizi wake katika kuratibu usalama na kwa kiasi kikubwa cha vifaa vya ulinzi vinavyoendelea kumiminika nchini Ukraine," alisema Lloyd Austin.

Kulingana na waziri huyo, jumla ya nchi zaidi ya 20 zimetangaza vifurushi vipya vya usaidizi wa kiulinzi, ambavyo vitajumuisha mizinga, makombora, mifumo ya ulinzi ya pwani, mizinga, magari ya kivita, na baadhi ya nchi zimeahidi kusaidia kutoa mafunzo kwa wanajeshi wa Ukraine.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani ameahidi kuwa wanachama wa muungano huo wataongeza uratibu wa kuimarisha na kukifanya kikosi cha wanajeshi cha Ukraine kuwa cha kisasa.

**RUSSIA KUKUZA ZAIDI UHUSIANO NA CHINA**

Waziri wa mambo ya nje wa Russia Sergei Lavrov, amesema kuwa nchi yake itaangalia pendekezo la nchi za Magharibi ili kuanzisha tena uhusiano, lakini kwa sasa mwelekeo zaidi utakuwa kwa China.

Lavrov alishutumu nchi za Magharibi kwa kuunga mkono "Russophobia" tangu Russia ilipoanzisha operesheni yake maalum ya kijeshi nchini Ukraine.

"Ikiwa Ulaya wanataka kutoa kitu katika suala la kuanzisha tena uhusiano, basi tutazingatia kwa umakini ikiwa tutaihitaji au la," Lavrov alisema katika hafla moja.

Alisema Russia lazima iache kutegemea kwa njia yoyote vifaa vinavyotoka Magharibi, lengo ni kuendeleza uhusiano na China.

Alisisitiza kwamba Russia ingependa kujitegemea na kuwa karibu na nchi ambazo zimejidhihirisha kuwa zinaaminika na hazichezi muziki wa waimbaji wengine.

"Ikiwa nchi za Magharibi zitabadilisha mawazo yao na kupendekeza aina fulani ya ushirikiano, basi tunaweza kuamua." Aliongeza.

**MWANADIPLOMASIA WA RUSSIA AJIUZULU**

Mwanadiplomasia wa Russia ameacha kazi yake kupinga vita vilivyoanzishwa na nchi yake dhidi ya Ukraine.

Boris Bondarev, ambaye alifanya kazi katika ubalozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa huko Geneva, aliiambia BBC kuwa alijua uamuzi wake huenda Russia ikamwona kama msaliti.

Lakini alisimama na kauli yake kuwa vita hivyo ni uhalifu dhidi ya watu wa Ukraine na Russia.

Katika barua yake iliyotumwa kwenye mitandao ya kijamii na kushirikishwa na wanadiplomasia wenzake, Bondarev, alieleza kuwa amechagua kukatisha maisha yake ya utumishi kwa miaka 20 kwa sababu hangeweza kushiriki tena katika aibu hiyo ya umwagaji damu.

"Wale ambao walianzisha vita hivi wanataka kitu kimoja tu,kusalia madarakani milele," aliandika **BBC**

# ESPANYOLA YAKABIDHIWA KOMBE LA UBINGWA WA BETIKA SODO LIGI

**Mwandishi Wetu**

ESPANYOLA imekabidhiwa kombe la ubingwa wa Ligi ya soka ya Mchangani (Betika Sodo Bingwa Ligi), huku ikiruhusu kipigo katika mechi yao ya mwisho kwenye Uwanja wa Msufini katika Kituo cha Dar es Salaam.

Mchezo huo ambao ulijaza mashabiki, Espanyola ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani, Kinondoni, iliduwazwa kwa kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Care Boys ambayo ilimaliza ligi hiyo ikiwa nafasi ya pili.

Kipigo hicho ni cha pili kwa Espanyola baada ya awali kufungwa bao 1-0 dhidi ya Hard Number, kabla ya Jumapili iliyopita kuduwazwa na Care Boys yenye maskani yake Kinondoni B ambayo ilimaliza ya pili ikiwa na pointi 27 na kuachwa kwa poiti moja na mabingwa hao.

Akikabidhi kombe kwa mabingwa, Meneja Programu wa Times FM, Amani Misana, ambaye aliambatana na mwakilishi wa Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika, Frola Chacha, alisema ligi hiyo imefanyika kwa mafanikio na timu zimeonyesha upinzani wa hali ya juu.

"Hamasa imekuwa kubwa na kadri siku zilivyosonga mbele ndivyo upinzani wa timu na hata mashabiki uliongezeka, tunazipongeza timu zote zilizoshiriki katika Kituo cha Dar es Salaam, lakini Espanyola kwa kubakisha ubingwa nyumbani," alisema.

Kampuni ya Betika ambayo ndiyo inadhamini ligi hiyo, ilitoa zawadi ya kombe na pesa taslimu Sh. 400,000 kwa bingwa, wakati mshindi wa pili Care Boys wakiondoka na Sh. 200,000 na Jaga FC iliyomaliza nafasi ya tatu iliondoka na Sh. 100,000.

Timu hizo pia sanjari na Hard Numbers, Smart Fighter, Swaz Inter na Morocco Square zilizawadia Sh. 100,000 kila moja kwa kushiriki ligi hiyo huku Khalid Yahaya wa Espanyoa akiibuka mfungaji bora.

Hussein Tajiri wa Care Boys alitwaa tuzo ya mchezaji bora na Ibrahim Ponela wa Espanyola akiondoka na tuzo ya kipa bora na kila mmoja aliondoka na Sh. 50,000 huku kikundi cha ushangiliaji cha Hard Numbers na kile cha Espanyola vikitangazwa vikundi bora vya ushangiliaji na kuondoka na Sh. 150,000.

Nelson Mwanuzi, Meneja Masoko wa Betika, alisema wamefarijika kuona ligi hiyo imeonyesha ushindani wa kweli kwenye soka la mchangani ambako mbali na Dar es Salaam, pia ilichezwa katika vituo vya Ruvuma, Lindi, Moshi, Iringa na Mwanza ambako kote mabingwa wa vituo hivyo wamepatikana.

"Tunaanza mchakato ili sasa mabingwa wa vituo vyote kuchuana ili kupata bingwa wa Taifa, mchakato huo utafanyika karibuni na utatangazwa," alisema.




Wachezaji wa Espanyola wakiwa na kikombe cha ubingwa wa Ligi ya Betika Sodo baada ya kuutwaa wiki hii. **MPIGAPICHA WETU.**

## Mabondia kuzipiga 'Usiku wa Kisasi' Dar

**Na Saada Akida**

MABONDIA kutoka B. Combination Gym, wanatarajia kushuka dimbani kurudisha heshima ya Mbagala katika 'Usiku wa Kisasi' utakaofanyika Juni 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa (Indoor Taifa), Dar es Salaam.

Mabondia watakaozichapa katika usiku huo ni Emmanuel Mwakyembe ambaye atazichapa dhidi ya Hamis Morinyo katika pambano la raundi nane kwenye 'Usiku wa Kisasi'.

Wengine watakaopanda ulingoni siku hiyo ni Bondia Abubakari Kihio, ambeye ametuma salamu za vitisho kwa mpinzani wake, Ally Kilongora kuwa atafanya kitu ambacho dunia nzima itashangazwa naye.

Katika usiku huo, pia bondia Jackson Malinyingi atapanda ulingoni dhidi ya Said Mkola, huku Omary Mpemba akizichapa na Ally Mgonjwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, bondia Antony Peter, alisema amejiandaa vizuri kuweka heshima ya Mbagala kwa kuwapiga wapinzani wao katika pambano hilo la Usiku wa Kisasi.

Alisema wanafanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya pambano la Usiku wa Kisasi kuhakikisha Mbagala inakuwa moto katika tasnia ya ngumu na kuifanya kata hiyo kuwa tishio kwa masumbwi.

"Tumejiandaa vizuri katika pambano hilo, tuko tayari kwa ajili ya bondia yeyote ambaye atakuja mbele yetu, malengo yetu makubwa ni kuweka heshima ya Mbagala kwa Wilaya ya Temeke," alisema.

Naye Mwandaaji wa Pambano hilo, Selemani Semunyu, alisema baada ya kumalizika kwa fainali ya Bingwa wa Kitaa, sasa wanaleta Usiku wa Kisasi wa mabondia wa B. Combination.

# Simba Queens kuongeza wapya sita tu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba Queens umeweka wazi idadi ya wachezaji wapya watakaowasajili kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa kwa Wanawake Ukanda wa CECAFA, inayotarajiwa kufanyika hapa nchini jijini Arusha, watakuwa sita tu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, alisema wamejifunza kilichotokea msimu uliopita na hawatakuwa tayari kurejea makosa hayo hasa katika suala la usajili kwani lengo lao ni kufanya vizuri katika michezo ya Ligi ya Mabingwa Ukanda wa CECAFA.

Alisema wako katika usajili wakilenga kuongeza wachezaji sita wapya ndani ya kikosi hicho, lakini hawatakuwa tayari kuona nyota wao muhimu wakiondoka kwenda kusajiliwa na wapinzani wao, Yanga Princess na Fountain Gate Princess.

Meneja huyo alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanawabakiza na kuwaongeza mikataba wachezaji waliomaliza ambao wako katika programu ya kocha wao, Sebastian Nkoma kwa ajili ya kuitumikia timu hiyo kwa msimu ujao na michuano hiyo ya kimataifa kwa Ukanda wa CECAFA.

"Msimu huu tumedhamiria kufanya kweli katika michuano hiyo, tangu niwapo na bado nikiwapo hakuna mchezaji yeyote wa Simba Queens ambaye ni staa atakuja Simba na kwenda kucheza timu pinzani, ilitokea huko nyuma tu kwa kufanya makosa, sasa hakuna kosa kama hilo tena," alisema Makanya.

Simba Queens imefanikiwa kutetea ubingwa huo msimu huu kwa kupoteza mchezo mmoja tu dhidi ya Yanga Princess.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUBAKI UNITED
ERIK ten Hag ameweka bayana kwamba, anataka mshambuliaji wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, kubaki Manchester United kwa msimu mwingine. ***(Metro)***

### JESUS KWA ARSENAL, SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur itapambana na wapinzani wao wa jiji moja la London, Arsenal katika kuwania kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25, kutoka Manchester City. ***(Telegraph)***

### STERLING AMULIKWA MADRID
REAL Madrid inataka kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, baada ya kumkosa nyota wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23. ***(Star)***

### FORSTER ANUKIA SPURS
TOTTENHAM Hotspur inakaribia kufikia makubaliano ya mkataba wa uhamisho wa bure na golikipa wa Southampton na England, Fraser Forster mwenye umri wa miaka 34. ***(Mail)***

### ARTETA KWA TIELEMANS
KIUNGO wa kati wa Leicester na Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, ni mmoja wa wachezaji wanaolengwa na kocha wa Arsenal, Mikel Arteta msimu huu wa majira ya joto. ***(Telegraph)***

### SABA KUUZWA ARSENAL
ARSENAL watajaribu kuwauza karibu wachezaji saba wa kikosi cha kwanza msimu huu wa majira ya joto, akiwamo beki wa Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 27, na kipa wa Ujerumani, Bernd Leno mwenye miaka 30. ***(Sun)***

### JUVENTUS YAMTAKA GABRIEL
JUVENTUS wamepiga hatua katika juhudi za kumsajili mlinzi wa Arsenal, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### AARONSON AWINDWA LEEDS
LEEDS United ipo tayari kumsajili kiungo wa kati wa kimataifa wa Marekani, Brenden Aaronson mwenye umri wa miaka 21, kutoka Red Bull Salzburg kwa pauni milioni 23 . ***(Times)***

### SPALLETTI AMZUIA KOULIBALY
KOCHA wa Napoli, Luciano Spalletti amesisitiza kuwa hawezi kumuuza mchezaj wa kimataifa wa Senegal anayenyatiwa na Chelsea, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 30. ***(Star)***

### HENRY AWANIWA WOLVES
KLABU ya Wolves inamtaka mshambuliaji, Thomas Henry mwenye umri wa miaka 27, ambaye anaichezea klabu ya Venezia ya Italia. ***(Matteo Moretto, Twitter)***

### ROTHWELL AJIWEKA SOKONI
TIMU za Bournemouth na Sheffield United zinamfuatilia kwa karibu kiungo wa kati, Joe Rothwell mwenye umri wa miaka 27, ambaye anaondoka Blackburn Rovers. ***(Yorkshire Live)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ATOA SABABU KUTAKA KUTUA LIVERPOOL

Haikuwa Real Madrid na PSG pekee, nilikuwa kwenye mazungumzo ya kuungana na Klopp...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amefichua kwamba, alikuwa na mazungumzo na Liverpool alipokuwa akitafakari chaguo lake, kabla ya kuamua kusaini tena Paris Saint-Germain.

Mbappe mwenye umri wa miaka 23, anachukuliwa kuwa mchezaji wa thamani zaidi kwenye soka duniani kwa sasa, na alipendekezwa kuondoka Ufaransa na kujiunga na Real Madrid mkataba wake ulipokamilika mwishoni mwa msimu huu.

Aliishia kuipa kisogo klabu yake anayoipenda sana ya utotoni akipendelea kubaki katika nchi yake, na kutia saini mkataba mpya ambao utamuweka Paris hadi 2025.

Ingawa wengi waliamini kuwa zilikuwa mbio za farasi wawili kati ya wababe hao wa Hispania na Ufaransa katika kumuwania, Mbappe amefichua katika mahojiano na TeleFoot kwamba, alikuwa na wazo la kuelekea kule Anfield.

"Haikuwa Real Madrid na PSG pekee - nilikuwa kwenye mazungumzo ya kuungana na Jurgen Klopp kule Liverpool," alisema.

"Nilizungumza na Liverpool kwa sababu ndiyo klabu inayopendwa zaidi na mama yangu - mama yangu anaipenda Liverpool," alisema. "Sijui kwa nini, itabidi umuulize.

"Ni klabu nzuri na (kwanza) tulikutana nao miaka mitano iliyopita. Nilipokuwa Monaco nilikutana nao. Ni klabu kubwa.

"Tulizungumza kidogo, lakini si sana ... bila shaka, ilikuwa kati ya Real Madrid na Paris Saint-Germain mwishoni."

Mshambuliaji huyo nyota pia alibainisha kwa nini aliamua kubadilisha mawazo yake ya kuelekea Madrid, akisema kwamba, kuondoka kwa uhamisho huru pale Paris Saint-Germain na kuwaacha wasipate chochote isingekuwa sawa.

"Kila mtu anajua nilitaka kuondoka kwenda Real Madrid mwaka jana, na nadhani lilikuwa chaguo zuri kuondoka mwaka jana," alisema. "Lakini sasa ni tofauti kwa sababu nilikuwa mchezaji huru.

"Nilikuwa mchezaji huru. Kama ningeondoka nilitakiwa kuondoka kama mchezaji mkubwa, lakini kuna sehemu ya hisia.

"Mimi ni Mfaransa na najua mimi ni muhimu nchini, na unapokuwa muhimu lazima ufikirie si tu juu ya mpira wa miguu, lakini juu ya maisha yako.

"Nitakuwa Ufaransa baada ya kumaliza kucheza soka. Nitaondoka hapa (PSG), nitakuwa na familia yangu, marafiki zangu.

"Kitu pekee ninachoweza kusema ni asante kwa mashabiki wote wa Real Madrid, na klabu, kwa sababu walinipa upendo wote.

"Inashangaza kwa sababu nilikuwapo kwa wiki moja tu nilipokuwa na umri wa miaka 14 (kufanya mazoezi). Niliwaambia kila la kheri kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 222,

MECHI KALI
POLISI TANZANIA
VERSUS
MTIBWA SUGAR
1 | 2.19
X | 2.68
2 | 3.71

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588 0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AMBAKISHA RONALDO MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag amesema Cristiano Ronaldo ni sehemu ya mipango yake, lakini kocha huyo mpya wa Manchester United bado hajaamua kama Harry Maguire ataendelea kuwa nahodha msimu ujao.

Kocha huyo wa zamani wa Ajax, Ten Hag aliteuliwa kuwa mrithi wa Ralf Rangnick mwezi uliopita kwa mkataba wa awali wa miaka mitatu na alianza kazi rasmi Old Trafford, Jumatatu.

Ten Hag anachukuwa usukani huo wakati timu ikimaliza msimu vibaya zaidi katika historia ya Ligi Kuu, na msimu wa 2021-22, umekuwa wa tano mfululizo bila ya kupata taji lolote.

Mholanzi huyo ana masuala kadhaa muhimu ya kushughulikia, bila kusahau mustakabali wa Ronaldo na mjadala mpana wa nani anafaa kuwa nahodha wa United.

Ronaldo alifunga mabao 24 katika mechi 38 alizoichezea United katika msimu wake wa kwanza katika klabu hiyo, ambayo ni 13 zaidi ya Bruno Fernandes anayefuatia.

Licha ya kuwafungia 'Mashetani Wekundu' hao mabao muhimu, nafasi ya Ronaldo ndani ya kikosi imetiliwa shaka.

Lakini alipoulizwa katika mkutano wake wa kutambulishwa na waandishi wa habari kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno ana jukumu la kucheza chini yake msimu ujao, Ten Hag alijibu: "Bila shaka".

Akihojiwa juu ya kile anachotarajia kwa Ronaldo, Ten Hag alijibu kwa urahisi: "Malengo".

Ronaldo aliwahi kuwa nahodha wa United wakati fulani msimu huu ambapo nahodha wao, Maguire hakuwapo, huku baadhi wakihoji kama beki huyo anafaa kuendelea kuvaa kitambaa hicho.

Rangnick hapo awali alipendekeza kwamba inapaswa kuwa chini ya wachezaji kupiga kura juu ya nani anafaa kuwa nahodha wa United kuanzia msimu ujao, ingawa Ten Hag anatarajiwa kuwa na uamuzi wa mwisho.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52, ambaye aliiongoza Ajax kutwaa mataji matatu ya Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, katika misimu yake minne kamili ya uongozi, alitoa maoni machache kuhusu hali hiyo Jumatatu.

"Msimu ujao ni msimu tofauti," alisema. "Harry amefanya kazi nzuri na ni mchezaji mzuri.

"Amepata mafanikio mengi na amechangia sana Manchester United, kwa hivyo ninatazamia kufanya kazi naye.

"Bado niko kwenye mchakato wa kufanya uchambuzi, ili kuweka mahitimisho, lakini natarajia kufanya kazi na wachezaji nilionao."

# Neuer ajifunga Bayern hadi 2024

**MUNICH, Ujerumani**

MANUEL Neuer ameongeza mkataba wa mwaka mmoja wa kuendelea kucheza Bayern Munich, unaomunganisha na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, hadi mwaka 2024.

Golikipa huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ameshinda mataji 10 ya Bundesliga akiwa na Bayern, pamoja na DFB-Pokals mara tano na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili.

Neuer amecheza mechi 472 tangu asajiliwe kutoka Schalke mwaka 2011, na mkataba wake mpya ulipotangazwa Jumatatu, alionyesha furaha yake kuendelea kuwa hapo Bavaria.

"Ninafuraha sana kwamba safari yangu inaendelea katika klabu ya FC Bayern," aliiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Tutakuwa na timu nzuri tena ambayo tunaweza kucheza nayo kwa kila taji.

"Kama kipa, nahodha na kiongozi, nataka kuwa tegemeo na jambo muhimu katika malengo yetu makubwa.

"Tunataka kupanua rekodi yetu ya ubingwa na kushinda tena Kombe la DFB na Ligi ya Mabingwa Ulaya."

,883,040

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/05/22 | 13:00 | Vegalta Sendai vs Fagiano Okayama | 2.52 | 3.11 | 2.62 |
| 02. 25/05/22 | 13:00 | V Varen Nagasaki vs JEF United Chiba | 2.38 | 2.76 | 3.15 |
| 03. 25/05/22 | 13:00 | Thespakusatsu vs Roasso Kumamoto | 2.62 | 2.96 | 2.62 |
| 04. 25/05/22 | 13:00 | Shimizu S Pulse vs FC Tokyo | 2.59 | 3.13 | 2.54 |
| 05. 25/05/22 | 13:00 | Cerezo Osaka vs Urawa Red Diamonds | 2.76 | 3.10 | 2.40 |
| 06. 25/05/22 | 13:30 | Ventforet Kofu vs Tokushima Vortis | 2.43 | 2.81 | 3.01 |
| 07. 25/05/22 | 19:00 | Kristiansund vs Tromso | 2.75 | 3.40 | 2.40 |
| 08. 25/05/22 | 22:00 | Roma vs Feyenoord | 2.29 | 3.35 | 3.00 |
| 09. 26/05/22 | 05:30 | LA Galaxy vs Los Angeles FC | 2.36 | 3.59 | 2.52 |
| 10. 26/05/22 | 20:00 | AJ Auxerre vs St Etienne | 2.47 | 3.14 | 2.84 |
| 11. 26/05/22 | 20:45 | Kayserispor vs Sivasspor | 2.58 | 3.16 | 2.53 |
| 12. 26/05/22 | 21:00 | Sarpsborg vs Molde | 2.46 | 3.47 | 2.63 |
| 13. 26/05/22 | 21:00 | Vitesse Arnhem vs AZ Alkmaar | 2.87 | 3.37 | 2.30 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 25/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5991 | Cerezo Osaka vs Urawa Red Diamonds | 2.76 | 3.10 | 2.40 |
| 13:30 | 1160 | FC Seoul vs Jeju Utd | 2.96 | 3.10 | 2.28 |
| 13:30 | 1910 | Nagoya Grampus vs Avispa Fukuoka | 2.07 | 2.82 | 3.80 |
| 13:30 | 5515 | Ventforet Kofu vs Tokushima Vortis | 2.30 | 2.83 | 3.21 |
| 14:00 | 1053 | Balcatta vs Stirling Lions | 5.03 | 4.45 | 1.48 |
| 14:00 | 3167 | Mbeya Kwanza FC vs Kagera Sugar | 2.55 | 2.65 | 3.04 |
| 16:00 | 1411 | FC Zvezda Perm vs Zenit Izhevsk | 1.27 | 5.40 | 9.80 |
| 16:00 | 3904 | Polisi Tanzania vs Mtibwa Sugar | 2.19 | 2.68 | 3.71 |
| 17:15 | 5548 | Al Dhafra vs AL Urooba | 1.63 | 3.89 | 4.38 |
| 17:30 | 1969 | Tallinna Kalev vs Parnu JK Vaprus | 2.40 | 3.65 | 2.65 |
| 18:00 | 2127 | Cagliari Youth vs Sampdoria Youth | 2.08 | 3.70 | 2.87 |
| 18:00 | 2774 | Frydek Mistek vs Znojmo | 2.18 | 3.65 | 2.72 |
| 18:00 | 2975 | WA Tlemcen vs ES Setif | 8.35 | 4.27 | 1.34 |
| 18:00 | 3926 | Sigma Olomouc B vs FC Slovan Rosice | 1.40 | 4.29 | 6.44 |
| 18:00 | 5100 | CS Sfaxien vs ES Sahel | 2.75 | 2.70 | 3.00 |
| 18:30 | 1342 | Velke Mezirici vs FC Vysocina Jihlava B | 1.44 | 4.67 | 5.25 |
| 18:30 | 1708 | Blansko vs SFK Vrchovina | 1.56 | 3.98 | 4.76 |
| 18:30 | 3398 | Unicov vs Vratimov | 1.31 | 5.25 | 6.80 |
| 18:30 | 5164 | Viktoria Otrokovice vs Slovacko B | 3.26 | 3.69 | 1.92 |
| 18:30 | 5236 | Erzurum BB vs Istanbulspor | 2.21 | 3.50 | 2.77 |
| 18:45 | 2600 | Ruch Chorzow vs Radunia Stezyca | 1.75 | 3.60 | 3.99 |
| 19:00 | 2982 | Bodo Glimt vs Stromsgodset | 1.39 | 4.88 | 6.57 |
| 19:00 | 3128 | Aalesunds vs Jerv | 1.45 | 4.47 | 6.16 |
| 19:00 | 4527 | Stabaek W vs Valerenga W | 7.60 | 5.40 | 1.33 |
| 19:00 | 4721 | Odd Ballklubb vs Sandefjord | 1.69 | 3.98 | 4.28 |
| 19:00 | 4807 | Hlucin vs Fastav Zlin B | 1.29 | 5.26 | 7.59 |
| 19:00 | 5295 | Arna-Bjornar W vs Kolbotn W | 3.02 | 3.66 | 2.02 |
| 19:00 | 5757 | Kristiansund vs Tromso | 2.75 | 3.40 | 2.40 |
| 19:00 | 5775 | Viking vs Ham-Kam | 1.34 | 5.17 | 7.35 |
| 19:30 | 2920 | Trans Narva vs Flora Tallinn | 13.56 | 7.36 | 1.12 |
| 19:30 | 4264 | Lunds BK vs Torns IF | 1.98 | 3.60 | 3.16 |
| 20:00 | 1257 | Hammarby Talang FF vs IFK Haninge | 2.65 | 3.60 | 2.40 |
| 20:00 | 1373 | IF Sylvia vs Sandvikens IF | 3.01 | 3.60 | 2.04 |
| 20:00 | 2063 | VFV Hildesheim vs FC Teutonia 05 | 2.73 | 3.17 | 2.39 |
| 20:00 | 2557 | SV Allerheiligen vs Union Vocklamarkt | 2.22 | 3.55 | 2.95 |
| 20:00 | 2756 | BK Forward vs IF Karlstad Fotboll | 6.20 | 4.50 | 1.45 |
| 20:00 | 2950 | AL Wahda Scc (UAE) vs Al Nasr Dubai | 1.84 | 3.41 | 3.80 |
| 20:00 | 3078 | Kolding IF vs Aarhus Fremad | 2.32 | 3.46 | 2.63 |
| 20:00 | 3243 | Catanzaro vs Padova | 2.38 | 2.97 | 2.92 |
| 20:00 | 3502 | Motala Aif vs Orebro Syrianska | 2.20 | 3.65 | 2.95 |
| 20:00 | 3933 | Sollentuna Utd FF vs FC Stockholm Internazionale | 2.10 | 3.70 | 3.10 |
| 20:00 | 5665 | Al Wasl Dubai vs Jazira Abu Dhabi | 1.95 | 3.51 | 3.31 |
| 21:00 | 1947 | Eyupspor vs Bandirmaspor | 2.28 | 3.26 | 2.82 |
| 21:00 | 2763 | Lillestrom vs Valerenga | 1.98 | 3.58 | 3.43 |
| 21:30 | 2064 | Wigry Suwalki vs LKP Motor Lublin | 2.57 | 3.10 | 2.57 |
| 21:45 | 2456 | FC Altona 93 vs FC Oberneuland | 2.40 | 3.22 | 2.68 |
| 22:00 | 2165 | Feralpisalo vs Palermo | 2.33 | 2.98 | 2.98 |
| 22:00 | 4815 | Roma vs Feyenoord | 2.29 | 3.35 | 3.00 |
| 22:30 | 5352 | Ittihad Tanger vs RS Berkane | 3.10 | 2.81 | 2.37 |
| 23:00 | 1803 | Chacaritas FC vs CD Alianza Cotopaxi | 2.19 | 2.92 | 3.31 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# NAMUNGO YAKUBALI KIPIGO, YASEMA NNE-BORA LAZIMA

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**



HUKU akieleza malengo yao ya kumaliza nafasi nne za juu bado yapo pale pale, Kocha Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amekubali kiroho safi kupoteza mechi kwa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, akisema ndiyo mpira na kuwapongeza wapinzani wao, akiahidi timu yake itafanya vema kwenye mechi zinazofuata.

Bao pekee kwenye mechi hiyo lilifungwa kwa mkwaju wa penalti na Mcha Hamisi ambalo lilitosha kuwafanya wenyeji kutoka uwanjani kifua mbele.

"Ukiondoa Yanga, hakuna timu yoyote kwenye ligi hii ambayo haijafungwa, mpira ni mchezo wa makosa, mpira umepigwa umemgonga mchezaji wangu kwenye mkono ikawa penalti, basi goli limefungwa, lakini vijana wangu wamecheza vizuri, hatukuweza kutumia nafasi hasa kipindi cha kwanza.

"Kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri, kipindi cha pili tukacheza vizuri sana, lakini wenzetu walituachia tumiliki mpira, nadhani kwa sababu walikuwa tayari wana bao, wameshinda tunawapongeza na huu ni mpira, bado mechi nne, azma yetu iko pale pale kushika nafasi ya nne au ya tatu," alisema Julio.

Naye Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Mohamed Muya, alisema malengo yao ya kushinda mechi hiyo yametimia.

"Malengo yetu leo (juzi) ni kushinda, tunashukuru vijana wamepambana, tumepata bao moja, sasa tunayo matuimaini ya kubakisha timu Ligi Kuu, mapambano yanaendelea," alisema kocha huyo.

Wakati Namungo ikisalia na pointi zake 37, Dodoma Jiji imefikisha jumla ya pointi 31, ikiwa kwenye nafasi ya 10 ya msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

# Mpole kumtimulia vumbi Mayele kesho?

**Na Mwandishi Wetu**




MBIO za kuwania Kiatu cha Dhahabu zitaendelea tena kesho wakati George Mpole atakaposhuka dimbani kuiongoza Geita Gold FC kuivaa Tanzania Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Mpole ambaye ana mabao 14 sawa na Fiston Mayele wa Yanga, wanachuana vikali katika mbio hizo za kumaliza kinara wa mabao kwenye ligi hiyo ambayo inaelekea ukingoni kwa sasa.

Yanga inaongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 64, 13 zaidi ya Simba iliyopo nafasi ya pili, tayari timu hizo zimeshuka dimbani mara 26, huku kwa Geita mchezo huo wa kesho ukiwa ndio wa 26 kwao.

Hivyo, kama Mpole atafunga kesho dhidi ya Tanzania Prisons inayoshika nafasi ya pili kutoka mkiani, atakuwa ameweka pengo kubwa kwa Mayele kwani tayari atakuwa mbele kwa mabao wakati timu zao zikiwa zimecheza mechi sawa.

Katika mbio hizo, wawili hao wanafuatiwa kwa karibu na Riliants Lusajo wa Namungo ambaye hadi sasa amecheka na nyavu mara 10, akifuatiwa na Abdul Sopu wa Coastal Union mwenye mabao tisa, huku Rogers Kola wa Azam FC akiwa na mabao nane nyuma yake.

Straika wa Simba, ambaye ametwaa kiatu hicho kwa misimu miwili akiwa na Wekundu wa Msimbazi hao, msimu huu ameshindwa kuonyesha makeke yake ya kucheka na nyavu kwani ana mabao saba tu sawa na mchezaji mwenza wa timu hiyo, Denis Kibu pamoja na Saido Ntibazonkiza wa Yanga.

Mbali na mbio hizo za ufungaji bora lakini, Mpole na wachezaji wenzake wanapambana vikali kuhakikisha Geita Gold inamaliza nafasi nne za juu ili kupata tiketi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao, ambao Tanzania itaingiza timu nne. Geita kwa sasa ipo nafasi ya tano ikiwa na pointi 35, moja nyuma ya Azam FC iliyopo juu yake kabla ya mechi za jana.

# Michezo

Jumatano Mei 25, 2022






Mbappe na sababu kutaka kutua Liver



Pablo

Nabi

# PABLO, NABI NI ZAIDI YA MBINU KIRUMBA FA

●●●Wamaliza kusomana, kocha wa Simba asema hatakubali kupoteza mataji yote mawili, lakini...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, juzi alikuwa miongoni mwa wapenzi wa soka waliojitokeza kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Bara kati ya Biashara United na Yanga, ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa CCM Kirumba, hiyo ikionekana ni njia mojawapo ya kuwasoma wapinzani wake kabla ya Jumamosi timu hizo kukutana kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA.

Mechi hiyo ilipigwa ikiwa ni siku moja baada ya kikosi chake cha Simba kupata matokeo kama hayo uwanjani hapo dhidi ya Geita Gold FC, huku Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, naye akiwa ni miongoni mwa walioshuhudia mechi hiyo ya Ligi Kuu pia.

Hata hivyo, baada ya Nabi kuisoma Simba, ambayo siku hiyo ilimpumzisha beki wake wa kati, Henoc Inonga, ambaye amekuwa akimnyima raha ya kutetema, mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, Wanajangwani hao nao juzi walipumzisha mastaa wao wengi.

Mastaa wa Yanga ambao walipumzishwa na Yanick Bangala, Khalid Aucho na Kibwana Shomari, ambaye amekuwa katika kiwango cha juu hivi karibuni.

Baada ya kumaliza kusomana, jana Pablo alimwambia mwandishi wetu kuwa ana kazi ya kufanya katika safu yake ya ushambuliaji kwa kuwapa mbinu za kiufundi kuweza kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza ili kupata mabao kwenye mechi hiyo Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), dhidi ya Yanga.

Kikosi cha Simba jana asubuhi kilianzia mazoezi gym ili kuweka miili yao sawa kabla ya jioni kujifua Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza, ikiwa ni maandalizi kuelekea mchezo huo dhidi ya Yanga utakaopigwa katika Uwanja wa CCM Kirumba.

Pablo alisema licha ya kuwapo kwa changamoto ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini wamepania kutetea Kombe la Shirikisho.

Alisema kulingana na ukubwa wa Simba ulivyo, aina ya mashindano wanayoshiriki anahitaji kuona kila mchezaji anakuwa kwenye ubora ikiwamo mechi za ligi zilizobaki na dhidi ya Yanga katika mchezo wa nusu fainali ya Shirikisho.

"Kuna makosa ambayo yamekuwa yakijirudia katika mechi dhidi ya Azam FC tulitengeneza nafasi na kushindwa kufunga, sasa tunafanyia kazi hilo kuhakikisha hatukosi vyote kwa msimu huu, tuhakikishe tukikosa ligi basi tunatetea Kombe la Shirikisho," alisema Pablo.

Alisema kwa namna hiyo wanatakiwa kuwekeza nguvu zao na kufanyika kazi mapungufu yao ili kupambana kuhakikisha wanashinda dhidi ya Yanga na kucheza fainali ya kombe hilo.

Pablo alisema hatakubali kirahisi kupoteza mataji yote, hivyo wanaingia vitani kuboreshwa madhaifu yao hasa safu ya ushambuliaji kuhakikisha wanakuwa makini na kumalizia nafasi wanazotengeneza kuzaa mabao.

## Mabeki Yanga sasa wawekwa kitimoto

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema atakaa na mabeki wake kufanya tathmini ya bao walilofungwa kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara juzi dhidi ya Biashara United, akidai kuwa ni jepesi na ambalo lilipaswa kufungwa kwenye mechi za mchangani za watoto na si Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Kaze raia wa Burundi alisema mabeki wake walifanya makosa makubwa, kwani wakati goli linafungwa kulikuwa na mabeki wawili tu ndani ya boksi.

"Haiwezekani tumeshafunga bao, halafu wanatufunga goli kwenye ndani ya boksi, na tupo wawili tu, ni makosa makubwa sana, tunapaswa kukaa na kutathmini hili. Bao kama hili wanafungwa watoto kwenye mechi za mchangani na si kwa timu kubwa kama Yanga na kwenye Ligi Kuu," alisema Kaze.

Lilikuwa ni bao la Mkenya Collin Opare dakika ya 77, akiunganisha krosi iliyochongwa na Mkenya mwenzake, Ambrose Awio, ikiwa ni dakika tatu tu baada ya Yanga kupata bao lililofungwa na Fiston Mayele, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

Akizungumzia mechi hiyo, Kaze alisema wangeweza kupata mabao matatu kipindi cha kwanza kama si umakini mdogo wa wachezaji wake.

"Naweza kusema tungeweza kushinda tangu mwanzo, tumepoteza nafasi tatu za kufunga, mechi za hivi ukishindwa kufunga mpaka mapumziko, unampatia nguvu ya kuzuia mpinzani, lakini tumepokea pointi moja, tumecheza na timu ambayo imetupatia ushindani mkubwa, tunaangalia mechi inayofuata," alisema.

Mrundi mwenzake Kocha Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati alisema kwa asilimia kubwa wachezaji wake walicheza kwa kufuata maelekezo, japo kuna wakati waliteleza na ndipo walipoadhibiwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >